Haliuzwi

JUNI 22, 2026

/islamicftz

Muharram 6 1448

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 589

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Kambi ya macho, 886 wapatiwa miwani, 238 wafanyiwa upasuaji





# Ziara ya CIFCA Azerbaijan yaifungulia Tanzania fursa IsDBI

- Mikutano ya IsDB Baku yazaa makubaliano ya dola bilioni 6
- Fedha za IsDB zaupa msukumo mradi wa SGR nchini Uganda

Mwenyekiti wa Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA), Aref Nahdi (kushoto) akibadilishana makabrasha na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDBI), Dkt Sami Suwailem baada ya kusaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo mbili.

## CIFCA yaongeza washirika watatu wa kimataifa Dubai

## Profesa Assad: Utafiti ndiyo njia ya kupata suluhisho la matatizo ya Waislamu



## Rais Mwinyi: Tuilinde misingi ya dini, maadili na umoja wa Taifa



## Sheikh Al Ahdal aonya wanaokataa Hadithi huku wakikubali Qur'an pekee wanapotosha Uislamu



## Nchi saba zailaumu Israel kwa mashambulizi ya misikiti

NA MWANDISHI WETU

# Ziara ya CIFCA Azerbaijan yaifungulia Tanzania fursa IsDBI

Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA) na Taasisi ya Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (Islamic Development Bank Institute – IsDBI) zimesaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) itakayoweka msingi wa kuimarisha elimu, tafiti, mafunzo na ujenzi wa uwezo katika sekta ya fedha za Kiislamu nchini Tanzania.

Makubaliano hayo yalitiwa saini Juni 19, 2026, pembezoni mwa Mikutano ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Group Annual Meetings 2026) iliyofanyika Baku, Azerbaijan.

Kwa mujibu wa MoU hiyo, CIFCA na IsDBI zitashirikiana katika kuhamasisha uelewa kuhusu fedha za Kiislamu, kuandaa programu za mafunzo, kujenga uwezo wa wataalamu, kufanya tafiti, kubadilishana uzoefu wa kitaalamu na kutekeleza shughuli nyingine zinazolenga kukuza maendeleo ya sekta hiyo nchini Tanzania.

Makubaliano hayo pia yanaweka mfumo rasmi wa ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili katika utekelezaji wa shughuli za pamoja za elimu, uhamasishaji na maendeleo ya sekta ya fedha za Kiislamu.

Akizungumza baada ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, Mwenyekiti wa CIFCA, ndugu Aref Mbarak Nahdi, alisema ushirikiano huo unafungua ukurasa mpya katika juhudi za kuendeleza mfumo wa fedha unaofuata misingi ya Kiislamu nchini kwa kuunganisha uzoefu wa kimataifa wa IsDBI na juhudi zinazofanywa na wadau wa ndani.

## Tanzania, nafasi ya kipekee

Nahdi alisema Tanzania ina nafasi ya kipekee katika maendeleo ya fedha za Kiislamu licha ya kutokuwa mwanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC), ambayo uanachama wake ni miongoni mwa masharti ya msingi kwa nchi kuwa mwanachama wa Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB).

Benki hiyo ina nchi wanachama 57 na moja ya masharti ya msingi ya kujiunga nayo ni kuwa mwanachama wa OIC. Hata hivyo, Nahdi alisema hali hiyo haijazuia Tanzania kujenga mahusiano na taasisi za Kundi la IsDB kupitia ushirikiano wa kitaalamu na maendeleo.

Nahdi alisema pamoja na Tanzania kutokuwa mwanachama wa OIC, nchi ina jamii kubwa ya Waislamu na fursa kubwa ya kukuza sekta ya fedha za Kiislamu, jambo linalofanya ushirikiano kati ya CIFCA na IsDBI kuwa muhimu katika kuiunganisha Tanzania na uzoefu wa kimataifa wa taasisi za Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu.

Nahdi alisema Tanzania ina fursa kubwa ya kunufaika na maendeleo ya fedha za Kiislamu na kwamba ili kufikia lengo hilo, CIFCA imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na wadau mbalimbali nchini, ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania (BoT), katika kukuza uelewa, elimu, tafiti, mafunzo, maendeleo ya miundombinu ya fedha za Kiislamu pamoja na mazingira wezeshi ya ukuaji wa sekta hiyo.

Mwenyekiti huyo wa CIFCA alisema anatarajia makubaliano hayo yataimarisha zaidi juhudi hizo kupitia ushirikiano wa kitaalamu na IsDBI, taasisi ambayo imejijengea sifa ya kuwa kitovu cha maarifa, tafiti na maendeleo ya fedha za Kiislamu katika Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu.

Nahdi alisema hatua inayofuata ni kutafsiri makubaliano hayo katika programu za vitendo zitakazowanufaisha wadau mbalimbali, ikiwemo taasisi za fedha, wasomi, wataalamu, wanafunzi, watunga sera na wadau wengine wa maendeleo.

Alisema maeneo yanayotarajiwa kupewa kipaumbele ni pamoja na mafunzo ya kitaalamu, tafiti, ujenzi wa uwezo wa rasilimali watu, ukuzaji wa maarifa kuhusu fedha za Kiislamu na kusaidia taasisi za Tanzania kunufaika na uzoefu wa kimataifa wa IsDBI.

Kwa upande wake, IsDBI iliyowakilishwa na Dkt Sami Suwailem, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa IsDBI, ilisisitiza umuhimu wa kuzingatia utekelezaji wa shughuli zenye matokeo yanayoonekana badala ya kuishia kwenye makubaliano ya maandishi pekee. Pande hizo mbili zilikubaliana kuanza kwa kutambua maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa kwa ushirikiano katika kipindi cha miaka ijayo.

## Apigia chapuo elimu, hamasa uchumi wa Halal Afrika

Awali, kabla ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, Nahdi alipata fursa ya kuzungumza katika moja ya vikao vya mkutano huo na kutoa wito kwa washirika wa maendeleo, hususan Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB), kuongeza juhudi za kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu uchumi wa Halal katika nchi za Afrika.

Alisema wananchi wengi bado wanafahamu Halal kama suala linalohusiana na vyakula pekee, wakati dhana hiyo inajumuisha pia biashara, uwekezaji, fedha za Kiislamu, utalii, vipodozi, dawa, usafirishaji na sekta nyingine za uchumi.

Nahdi alisema tofauti na nchi kama Malaysia, Saudi Arabia na mataifa mengine ya Mashariki ya Kati ambako uelewa kuhusu Halal ni mkubwa, nchi nyingi za Afrika bado zinahitaji kampeni za elimu na uhamasishaji ili wananchi waweze kunufaika na fursa zinazotokana na uchumi wa Halal unaokua kwa kasi duniani.

Alieleza kuwa Afrika ina idadi kubwa ya vijana na inaendelea kuwa kitovu muhimu cha ukuaji wa uchumi wa dunia, jambo linaloifanya kuwa na nafasi ya kipekee katika maendeleo ya sekta ya Halal ikiwa itawekewa mazingira mazuri ya elimu na uelewa.

Nahdi alisisitiza kuwa kuongeza uelewa kuhusu Halal barani Afrika kutasaidia kufungua fursa mpya za uwekezaji, biashara na ajira, huku akiwataka wadau wa sekta hiyo kushirikiana kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wananchi katika maeneo mbalimbali ya bara hilo.

## Hatua nyingine kubwa kwa CIFCA

Akizungumzia kuhusu makubaliano yaliyofikiwa kati ya CIFCA na IsDB, Mwenyekiti Mtendaji wa Yusra Sukuk Company Limited alisema mafanikio hayo ni sehemu ya mkakati mpana wa CIFCA wa kujenga mahusiano na taasisi za kimataifa ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2021.

Alisema katika kipindi hicho CIFCA imefanikiwa kusaini makubaliano ya ushirikiano wa kimkakati na taasisi mbalimbali za kimataifa zinazotambulika katika sekta ya fedha za Kiislamu.

مُحرم



# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha Wetu

AZERBAIJAN

# Mikutano ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Group Annual Meetings 2026) iliyofanyika Baku, Azerbaijan




Mwenyekiti wa Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA), Aref Nahdi akihutubia katika mikutano ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Group Annual Meetings 2026) iliyofanyika Baku, Azerbaijan










NA MWANDISHI WETU

# Rais Mwinyi: Tuilinde misingi ya dini, maadili na umoja wa Taifa

■ **Asema ujio wa mwaka mpya wa Kiislamu unapaswa kuwa fursa ya kutafakari upya wajibu wa kila mmoja katika kujenga jamii yenye mshikamano, heshima na maadili mema.**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wananchi kuufanya Mwaka Mpya wa Kiislamu 1448 Hijria kuwa mwaka wa kuimarisha maridhiano, upendo, ustahamilivu na mshikamano, akisisitiza kuwa amani na umoja ni nguzo muhimu za maendeleo ya Taifa.

Rais Dkt. Mwinyi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza katika Maadhimisho ya Mwaka Mpya wa Kiislamu yaliyofanyika katika Msikiti wa Jamiu Zinjibar, Kiembe Samaki, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Katika salamu zake kwa wananchi, Rais Mwinyi alisema ujio wa mwaka mpya wa Kiislamu unapaswa kuwa fursa ya kutafakari upya wajibu wa kila mmoja katika kujenga jamii yenye mshikamano, heshima na maadili mema.

Aliwataka wananchi kuendelea kuheshimiana, kuvumiliana na kujiepusha na vitendo au kauli zinazoweza kusababisha migawanyiko ndani ya jamii.

"Tunapaswa kuufanya mwaka huu kuwa wa maridhiano, upendo na ustahamilivu, kwa sababu amani na umoja wetu ndiyo msingi wa maendeleo tunayoyahitaji," alisema Rais Mwinyi.

Alisisitiza kuwa maendeleo ya Taifa hayawezi kupatikana bila kuwepo kwa mazingira ya amani, ushirikiano na kuheshimiana miongoni mwa wananchi.

Rais Mwinyi amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za dini katika kuimarisha amani, maadili na ustawi wa jamii.

Ameeleza kuwa taasisi za dini zina mchango mkubwa katika malezi ya jamii kwa kuhimiza maadili mema, mshikamano na uwajibikaji miongoni mwa wananchi.

Aidha, Rais Mwinyi alipongeza Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar pamoja na wadau wote waliohusika katika maandalizi ya maadhimisho hayo kwa kufanikisha hafla hiyo.

Pia aliwapongeza viongozi wa dini kutoka nchi mbalimbali za Afrika Mashariki walioshiriki katika maadhimisho hayo, akisema ushiriki wao unaonyesha umuhimu wa kuendeleza umoja na ushirikiano wa kidini na kijamii katika ukanda huo.

Maadhimisho ya Mwaka Mpya wa Kiislamu 1448 Hijria yamefanyika wakati ambapo viongozi mbalimbali wa dini na wananchi walikusanyika kwa ajili ya dua, mawaidha na tafakari kuhusu umuhimu wa amani, mshikamano na kuendeleza maadili katika jamii.

Katika hatua nyingine, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza Jumatano, tarehe 17 Juni 2026, kuwa siku ya mapumziko kwa ajili ya kuadhimisha Mwaka Mpya wa Kiislamu 1448 Hijria.

Tangazo hilo limewapa wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu katika matukio mbalimbali ya kumbukumbu ya mwaka huo mpya wa kalenda ya Kiislamu.

Kwa ujumla, ujumbe mkuu wa Rais Mwinyi katika maadhimisho hayo umejikita katika kuhimiza jamii kuendeleza misingi ya amani, upendo na mshikamano kama njia ya kujenga Zanzibar yenye utulivu na maendeleo endelevu.



NA MWANDISHI WETU

# SHEIKH AL AHDAL AONYA:
# "Wanaokataa Hadithi huku wakikubali Qur'an pekee wanapotosha Uislamu"

**Amesema baadhi ya watu wamekuwa wakijaribu kumtenganisha Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) kwa kukataa Hadithi, wakisisitiza kuwa wao wanakubali Qurani pekee bila Sunna.**

Waislamu wametakiwa kuwa makini na watu wanaodai kuamini Qurani pekee huku wakipinga Hadithi (Sunna) za Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake), wakielezwa kuwa msimamo huo unapingana na msingi wa mafundisho ya Kiislamu.

Akitoa Khutuba ya Ijumaa Juni 19, 2026 katika Msikiti wa Jamiul Nurul Hikma, Sheikh Abdulqadir Shariff Al Ahdal amesema wapo baadhi ya watu wanaotumia mitandao ya kijamii kutafuta umaarufu kwa kueneza mitazamo inayopotosha uelewa sahihi wa dini.

"Hawa ninawafananisha na mtu aliyeamua kukojoa kwenye kisima maarufu cha maji ya Zamzam wakati wa Hijjah kwa lengo la kupata umaarufu. Hivyo hawa nao wanakojoa mitandaoni kwa kutafuta umaarufu," amesema Sheikh Al Ahdal.

Amesema baadhi ya watu wamekuwa wakijaribu kumtenganisha Mwenyezi Mungu na Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) kwa kukataa Hadithi, wakisisitiza kuwa wao wanakubali Qurani pekee bila Sunna.

### Mtume alitabiri zama zitafika ambazo watu watakataa Hadithi zake

Sheikh Al Ahdal amesema Mtume Muhammad alitabiri kuwa kutakuja kipindi ambacho baadhi ya watu watakataa Hadithi zake.

### Amefafanua kuwa Hadithi zinajumuisha:

Huku akitaja aya kadhaa za Qurani na Hadithi za Mtume, Sheikh amewakumbusha Waislamu kwamba Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) hakuwa akisema kwa matamanio yake, bali kwa ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. .

### "Qurani na Sunna haviwezi kutenganishwa"

Akirejea aya mbalimbali za Qurani, Sheikh huyo amesema Waislamu wanatakiwa kuwaamini Mitume wote waliotumwa na Mwenyezi Mungu pamoja na mafundisho yao.

**Ametaja aya za:**

**An-Nisaa 4:150–152** — zinazosisitiza umuhimu wa kuwaamini Mitume wote.

**An-Nahl 16:44 na 16:64** — zinazoeleza kuwa jukumu la Mtume halikuwa kufikisha Qurani pekee, bali pia kuifafanua na kuieleza kwa watu.

Ametoa mfano wa ulaji wa samaki akisema kuwa baadhi ya mambo hayawezi kueleweka bila ufafanuzi wa Mtume.

"Mkiwa mnajadili jambo fulani, halafu mtu akasema, 'Ninataka unipe aya ya Qurani pekee, sitaki Hadithi,' muulizeni: 'Unakula samaki?' Akijibu, 'Ninakula,' muulizeni 'ni nini kinachokufanya ule samaki wakati Qurani inasema msile vitu vilivyokufa bila kuchinjwa?' Kimsingi kinachotufanya tule samaki ni ufafanuzi uliotolewa na Mtume Muhammad (SAW), lakini kwa kutegemea Qurani pekee huwezi kula samaki," amesema.



### Swala na mazishi: Mifano ya umuhimu wa Sunna

Sheikh Al Ahdal amesema Qurani imetaja mambo mengi kwa ujumla, huku maelezo yake yakapatikana kupitia Hadithi za Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake).

Ametolea mfano:

Swala — Qurani imeamrisha kuswali, lakini haijaeleza kwa kina idadi ya rakaa na muda wa kila swala.


Mazishi — Qurani imeelekeza mtu akifa azikwe, lakini taratibu za mazishi zimefafanuliwa kupitia Sunna za Mtume Muhammad (Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake).

Amehimiza Waislamu kujifunza dini kutoka katika vyanzo vyake sahihi na kutokubali mafundisho yanayojengwa kwa kutafuta umaarufu badala ya ukweli wa dini.

مُحرم

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI WETU



# Profesa Assad: Utafiti ndiyo njia pekee ya kupata suluhisho la matatizo ya Waislamu

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro (MUM), Profesa Mussa Assad, ametoa wito kwa wanazuoni, taasisi za elimu ya juu, viongozi wa dini na jumuiya za Kiislamu kuwekeza zaidi katika tafiti na ukusanyaji wa takwimu sahihi ili kusaidia kufanya maamuzi yenye msingi wa ushahidi badala ya makadirio.

Profesa Assad alisema jamii nyingi, ikiwemo Jumuiya ya Waislamu, inakabiliwa na changamoto ya kufanya maamuzi bila kuwa na taarifa sahihi kuhusu mahitaji, hali na idadi ya watu wanaowahudumia.

Akizungumza katika hafla moja ya kijamii, Profesa Assad alisema hakuna njia mbadala ya kupata uelewa sahihi wa hali halisi ya jamii isipokuwa kufanya tafiti za kina na kujenga mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa taarifa.

"Wito wangu ni kuwa hakuna namna nyingine zaidi ya kufanya tafiti. Lazima tufanye tafiti ili kupata data sahihi. Kama uko chuo kikuu lazima ufanye tafiti," alisema.

Profesa Assad, ambaye pia ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa zamani wa Hesabu za Serikali (CAG), alisema vyuo vikuu vinapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuzalisha maarifa yatakayosaidia kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

Alitolea mfano sekta ya elimu ya dini akisema hadi sasa hakuna takwimu sahihi zinazoonyesha idadi ya madrasa nchini, walimu waliopo, mitaala inayotumika wala mazingira ya wanafunzi wanaosoma katika taasisi hizo.

"Sasa hivi idadi ya madrasa haijulikani, madrasa gani iko wapi, ina walimu gani, ina mtaala gani wanatumia na watoto wanaosoma humo wanatoka katika mazingira gani. Ukikusanya data hizo ndipo unaweza kujua mahitaji halisi, kama tunahitaji walimu wangapi au mtaala wa aina gani," alisema.

Alisema takwimu zinaipa jamii uwezo wa kuzungumza kwa hoja mbele ya mamlaka na kupanga kwa usahihi mipango ya maendeleo.

Profesa Assad pia aliwataka maimamu na viongozi wa misikiti kuanza kujenga utamaduni wa ukusanyaji wa taarifa katika maeneo yao badala ya kujikita katika shughuli za ibada pekee.

"Data kwa rai yangu ianzie msikitini. Ukishakuwa Imam sio kusalisha tu, kusanya takwimu za watu wako, ujue una Waislamu wangapi, wanaishi wapi na mahitaji yao ni yapi," alisema. Alisema uwepo wa takwimu sahihi unaweza kusaidia hata katika utekelezaji wa shughuli za kijamii na misaada kwa kutambua watu wanaostahili kunufaika badala ya kutumia makadirio.

"Data ni muhimu sana katika mambo yetu yote ya ibada na yasiyo ya ibada. Waislamu tukae vizuri tukusanye data zetu," alisisitiza.

مُحرم

KALAMU HURU

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323



# Hatari ya maasi na upotevu wa muda katika ushabiki wa soka

Ndugu msomaji, umewahi kujiuliza kiwango cha muda unaoutumia kufuatilia ligi za mpira wa miguu, mechi za kimataifa au mijadala ya timu unayoishabikia? Je, muda huo unaoupoteza unakuletea manufaa ya kweli katika maisha yako ya kila siku au unakupotezea fursa muhimu ambazo hazirejei tena?

Katika maisha ya mwanadamu, hakuna kitu chenye thamani kubwa kama muda. Mali inaweza kupatikana tena baada ya kupotea, lakini dakika moja ikishapita haiwezi kurudi.

Mafundisho ya dini ya Kiislamu yanahimiza mtu kutumia ujana wake, afya yake, utajiri wake na nafasi yake katika mambo yenye manufaa kabla ya kufikwa na hali zinazoweza kumzuia kufanya hivyo.

Hata hivyo, katika zama hizi za teknolojia na matangazo ya moja kwa moja, mamilioni ya watu hutumia muda mwingi kufuatilia michezo mbalimbali hususan ligi za soka. Wengine huacha shughuli zao muhimu, huahirisha majukumu ya kifamilia, na hata hukimbizana kwa haraka ili wasikose mwanzo wa mechi wanayoisubiri.

## Swali muhimu

Swali la kujiuliza ni hili: Je, ushabiki huu umebaki ni burudani yenye tija au umegeuka uraibu unaotawala maisha ya watu wengi na kuwaingiza katika hatari ya maasi na upptevu wa muda?

Miongoni mwa changamoto zinazotajwa na wanazuoni wa Kiislamu ni matumizi makubwa ya muda katika kufuatilia mechi, uchambuzi na mijadala ya timu huku watu wakipunguza muda wa ibada, masomo, kazi au hata mazungumzo na familia yake.

Changamoto nyingine ni matumizi ya fedha. Katika baadhi ya mazingira, ushabiki wa soka umeambatana na kamari na ubashiri wa matokeo ya mechi. Watu huweka dau wakitarajia kupata faida iwapo timu wanazozipenda zitashinda. Kwa mtazamo wa Uislamu, vitendo vya aina hiyo vimekatazwa kwa sababu vinaingia katika mlango wa kamari.

Aidha, mechi nyingi huandamana na burudani mbalimbali, muziki na maonesho ambayo baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa yanapingana na maadili ya Kiislamu. Wapo pia wanaohofia kuwa mazingira hayo yanaweza kuwafanya watu kupuuza mipaka ya dini katika mavazi, mazungumzo na mahusiano.

Ushabiki uliopitiliza pia unaweza kuzaa migogoro isiyo na sababu. Mara nyingi mashabiki wa timu tofauti huingia katika mabishano makali, matusi na chuki zinazoweza kuharibu udugu na mahusiano yao. Wakati mwingine tofauti za kimichezo hubadilika na kuwa uhasama wa kweli kati ya watu ambao kwa kawaida walipaswa kuishi kwa amani na kuheshimiana.

Jambo lingine linalozua mjadala ni tabia ya baadhi ya vijana kuiga kila kitu kinachofanywa na wachezaji wanaowapenda. Kuanzia mitindo ya nywele, mavazi, mienendo na hata baadhi ya alama au ishara zinazotokana na tamaduni tofauti na zile za Kiislamu. Wazazi wengi wamekuwa wakihofia athari za kuigwa kwa watu mashuhuri bila kuchunguza kwanza maadili na misingi wanayoiwakilisha.

## Haijakatazwa moja kwa moja kutazama

Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya mchezo wa soka kuucheza au kuutazama ni jambo lililokatazwa. Baadhi ya wanazuoni wameeleza kwamba mchezo huo unaweza kuwa halali iwapo hautahusisha kamari, hautamzuia mtu kutekeleza wajibu wake wa kidini, na hautakuwa na mambo yaliyoharamishwa kama kufichua uchi, matusi au maovu mengine.

Kwa hiyo, tatizo si soka lenyewe, bali namna linavyotazamwa na nafasi linayopewa katika maisha ya mtu.

Ndugu msomaji, ni vyema kila mmoja wetu akajitathmini. Je, soka ni burudani inayokuongezea nguvu baada ya kazi na majukumu yako, au limekuwa sababu ya kupoteza muda, fedha na kuharibu maadili? Jibu la swali hilo linaweza kukusaidia kupanga upya vipaumbele vyako na kutumia vizuri neema ya muda uliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Mwisho wa yote, burudani inahitajika katika maisha, lakini haipaswi kuwa kubwa kuliko wajibu. Mafanikio ya kweli hayapatikani kwa kujua matokeo ya kila mechi, bali kwa kutumia muda wetu katika yale yanayotuletea manufaa duniani na Akhera.



NA MWANDISHI WETU

# Kambi ya macho yarejesha matumaini kwa 2,168

## ■ 886 wapatiwa miwani ■ 238 wafanyiwa upasuaji

Jumla ya wananchi 2,168 wamefanyiwa vipimo vya macho katika kambi ya matibabu iliyoandaliwa na taasisi ya The Islamic Foundation, ambapo kati yao 238 wamefanyiwa upasuaji bila malipo, huku wagonjwa 886 wakipatiwa miwani za kusomea kulingana na ukubwa wa matatizo yao. Zaidi ya wananchi 1,000 pia walipatiwa dawa mbalimbali.

Takwimu hizo zimetolewa na msimamizi mkuu wa kambi hiyo, Mussa Buluki, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa taasisi ya The Islamic Foundation, baada ya kuhitimishwa kwa kambi ya siku nne iliyohusisha timu ya madaktari bingwa kutoka Wizara ya Afya.

Kambi hiyo ilifadhiliwa na Shirika la Mercy Outreach Global la Uingereza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya, ikiwa na lengo la kurejesha tabasamu kwa jamii inayokabiliwa na changamoto za macho.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa kambi hiyo iliyofanyika katika Kituo cha Al-Jamih for Mother and Child Health Care kilichopo Msamvu mkoani Morogoro, Buluki alisema kambi hiyo imepata mafanikio makubwa licha ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utoaji wa huduma, huku ikiwavutia wagonjwa wengi kutoka maeneo mbalimbali, ikiwamo mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Alifafanua kuwa ndani ya kipindi cha miezi sita, taasisi ya The Islamic Foundation imefanikiwa kuandaa kambi mbili za matibabu ya macho, hatua ambayo inaonesha uhai na dhamira ya taasisi hiyo katika utoaji wa huduma za afya kwa jamii.

"Vituo vyetu vya kutoa huduma za afya kwa muda mrefu vilikuwa vimefungwa kwa ajili ya maboresho. Hivyo, kambi hizi ambazo zimepata mwitikio mkubwa wa wananchi zinarejesha imani ya jamii kwa taasisi katika utoaji wa huduma za afya," alisema Buluki.

Aliongeza kuwa mahitaji ya huduma za macho katika jamii bado ni makubwa, jambo linalothibitishwa na idadi kubwa ya watu waliojitokeza kutoka maeneo mbalimbali kutafuta huduma hizo.

"Kitu ambacho tumekiona ni kwamba jamii ina uhitaji mkubwa sana wa huduma hizi za macho, kwani wingi wa watu waliokuja kutoka maeneo mbalimbali unadhihirisha kuwa wengi wanashindwa kumudu gharama za matibabu," alisema.

Buluki aliushukuru uongozi wa taasisi ya The Islamic Foundation chini ya Mwenyekiti wake, Aref Nahdi, kwa kufanikisha utolewaji wa huduma hizo za matibabu, huku akitoa wito wa kutafutwa kwa wafadhili zaidi ili kuendeleza huduma hizo ambazo zimeleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Aidha, aliwashukuru vijana 78 wa kujitolea wa The Islamic Foundation (TIF Volunteers) kwa kujituma katika utekelezaji wa shughuli za kambi hiyo na kuwasihi kuendelea na moyo huo wa kujitolea, akieleza kuwa kazi wanayoifanya ina malipo makubwa mbele ya Allah.



DUBAI, (UAE)

NA MWANDISHI WETU

# CIFCA yaongeza washirika watatu wa kimataifa Dubai

Wakati wengi walipokuwa wakihitimisha ushiriki wao katika Mikutano ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) nchini Azerbaijan na kurejea nyumbani, ujumbe wa Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA) ulielekea Dubai kutafuta fursa mpya za maendeleo ya sekta ya fedha imayofuata misingi ya Kiislamu nchini Tanzania.

Hatua hiyo imezaa matokeo mapya baada ya CIFCA kusaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano wa Kimkakati (MoU) na Noor Shariah Technologies Solutions ya Falme za Kiarabu (UAE), huku pia ikifikia makubaliano ya mafunzo na mkufunzi wa kimataifa wa Shirika la Uhasibu na Ukaguzi wa Taasisi za Fedha Zinazofuata Misingi ya Kiislamu (AAOIFI), Safina Shahid, na kufungua mazungumzo ya ushirikiano na Al-Hadi Shariah Advisors.

Makubaliano hayo na Noor Shariah yalitiwa saini Juni 21, 2026 jijini Dubai na Mwenyekiti wa CIFCA, Aref Nahdi, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Noor Shariah Technologies Solutions, Dkt. Uzair Usmani.

Noor Shariah ni taasisi ya kimataifa yenye makao makuu Dubai inayotoa huduma za ushauri wa Shariah, utawala bora, usimamizi wa vihatarishi, ukaguzi wa ndani, teknolojia za fedha (FinTech), ushauri wa uwekezaji na huduma nyingine za kitaalamu katika sekta ya fedha.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, taasisi hizo mbili zitashirikiana katika mafunzo ya benki na fedha za Kiislamu, ushauri wa Shariah, utawala bora, usimamizi wa hatari, ukaguzi wa ndani, uzingatiaji wa sheria na viwango vya kimataifa pamoja na huduma za teknolojia ya fedha.

Maeneo mengine ya ushirikiano ni pamoja na ushauri wa miamala ya uwekezaji, uchambuzi wa takwimu, huduma za FinTech, pamoja na ushauri kuhusu viwango vya kimataifa vya taarifa za fedha (IFRS) na viwango vya uhasibu vya sekta ya umma (IPSAS).

Makubaliano hayo pia yanakusudia kuimarisha uwezo wa taasisi za fedha nchini Tanzania kwa kuzifikishia huduma za kitaalamu na uzoefu wa kimataifa unaotolewa na Noor Shariah katika masoko mbalimbali duniani.

## Mafunzo ya Ukaguzi wa Shariah na AAOIF

Mbali na kusaini MoU hiyo, viongozi wa CIFCA walifanya mkutano na Safina Shahid, mkufunzi mwenye ithibati za kimataifa kutoka AAOIFI katika eneo la Ukaguzi wa Shariah (Shariah Audit).

Safina ana uzoefu mkubwa katika ukaguzi wa ndani, ukaguzi wa nje na usimamizi wa vihatarishi baada ya kufanya kazi katika taasisi mbalimbali za fedha za kimataifa na kampuni zinazounda kundi la Nne Bora (Big Four) katika sekta ya ukaguzi wa hesabu.

Kufuatia mazungumzo hayo, CIFCA imeafikiana kuingia katika makubaliano ya ushauri binafsi na Safina Shahid kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Ukaguzi wa Shariah kwa wadau wa sekta ya fedha za Kiislamu nchini Tanzania.

Hatua hiyo inatarajiwa kusaidia kuimarisha viwango vya uzingatiaji wa Shariah, ukaguzi wa ndani na utawala bora katika taasisi za kifedha zinazotoa huduma za fedha za Kiislamu.

Katika hatua nyingine, viongozi hao pia walikutana na Al-Hadi Shariah Advisors kwa lengo la kuchunguza maeneo ya ushirikiano yatakayowezesha taasisi hizo kutumia uzoefu wao katika kukuza sekta ya fedha za Kiislamu nchini Tanzania, Afrika Mashariki na maeneo mengine ya bara la Afrika.

## Baku hadi Dubai: Imekuwa ziara ya mafanikio

Ndani ya kipindi cha chini ya wiki moja, CIFCA imefanikiwa kusaini Hati ya Ushirikiano na IsDB Institute nchini Azerbaijan, kusaini MoU ya kimkakati na Noor Shariah Technologies Solutions nchini UAE, kufikia makubaliano ya mafunzo ya Shariah Audit na mkufunzi wa kimataifa wa AAOIFI, pamoja na kufungua mazungumzo ya ushirikiano na Al-Hadi Shariah Advisors.

Akizungumza baada ya shughuli hizo, Katibu Mkuu wa CIFCA, Salum Lupande, alisema mafanikio hayo ni matokeo ya juhudi za muda mrefu za kujenga mahusiano ya kimataifa zilizoanza mwaka 2025 wakati wa Mkutano wa Pamoja wa IsDB na AAOIFI uliofanyika Manama, Bahrain.



Alisema katika mkutano huo alipata fursa ya kukutana na viongozi wa Noor Shariah kwa mara ya kwanza kabla ya kutembelea ofisi zao jijini Dubai, hatua iliyoweka msingi wa ushirikiano uliorasimishwa sasa.

Lupande alisema matokeo ya ziara za Baku na Dubai yanaonesha namna ushiriki wa CIFCA katika majukwaa ya kimataifa unavyoendelea kuzaa matunda kwa Tanzania.

Kwa mujibu wake, mafanikio hayo yanalenga kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani, kuimarisha taasisi za fedha za Kiislamu, kuvutia uwekezaji na kuiweka Tanzania katika nafasi bora ya kuwa kitovu cha maendeleo ya fedha za Kiislamu katika Afrika Mashariki.

UKHTI FATIMA SS




# Mikutano ya IsDB Baku yazaa makubaliano ya dola bilioni 6




***BAKU, Azerbaijan***

Mikutano ya 51 ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Group) iliyofanyika Baku, Azerbaijan imehitimishwa kwa kutiwa saini kwa makubaliano 67 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 6 pamoja na kuidhinishwa kwa ufadhili mpya wa dola bilioni 2.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika nchi wanachama.

Akizungumza katika mkutano wa kufunga mikutano hiyo Juni 19, Rais wa Kundi la IsDB, Dk. Muhammad Al Jasser, alisema mikutano hiyo imewakutanisha zaidi ya washiriki 4,400 kutoka nchi 78, wakiwemo viongozi wa taasisi 46 za kimataifa, kujadili masuala ya biashara, miundombinu, usalama wa chakula, fedha za Kiislamu, maendeleo ya sekta binafsi, mabadiliko ya tabianchi na mageuzi ya kidijitali.

“Mikutano ya mwaka mara nyingi hukumbukwa kwa hotuba zinazotolewa, lakini thamani yake halisi ipo katika kasi ya utekelezaji wa miradi na ushirikiano unaozaliwa kutokana na majadiliano hayo,” alisema Dk. Al Jasser.

Alisema katika kipindi cha siku nne za mikutano hiyo, zaidi ya vikao na matukio 32 ya ngazi za juu vilifanyika chini ya kaulimbiu ya “Ushirikiano wa Kikanda kwa Ustawi Endelevu”, yakihusisha viongozi wa serikali, wataalamu, wasomi na sekta binafsi kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Miongoni mwa makubaliano yaliyosainiwa ni pamoja na ufadhili wa dola milioni 234.8 kwa ajili ya kuboresha barabara ya Tafiré–Ferkessédougou nchini Côte d’Ivoire, dola milioni 59.3 kwa mradi wa umeme vijijini nchini Mauritania, dola milioni 20 kwa mradi wa mageuzi ya elimu nchini Chad na dola milioni 31 kwa mradi wa kuboresha uzalishaji wa mifugo nchini Gambia.

Benki hiyo pia ilizindua Mfumo wa Ushirikiano wa Kitaifa wa Somalia wenye thamani ya dola milioni 45 kwa kipindi cha 2026–2028 pamoja na kusaini makubaliano mengine ya maendeleo nchini Bahrain, Palestina na Sudan.

Dk. Al Jasser alisema ufadhili mpya wa dola bilioni 2.8 ulioidhinishwa wakati wa mikutano hiyo utasaidia miradi inayolenga kuimarisha miundombinu, usalama wa nishati, mifumo ya chakula, ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika nchi wanachama.

Alisema IsDB itaendelea kutumia ushirikiano, mshikamano na fedha za maendeleo kama nyenzo muhimu za kusaidia ustawi wa nchi wanachama na jamii za Kiislamu duniani.

## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS




# Fedha za IsDB zaupa msukumo mradi wa SGR Uganda

***KAMPALA, Uganda***

Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) imeidhinisha ufadhili wa euro milioni 650.75, sawa na takribani Sh trilioni 2.6 za Uganda, kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR), hatua inayotajwa kuwa ufadhili mkubwa zaidi kuwahi kutolewa na benki hiyo kwa mradi mmoja nchini humo.


Uamuzi huo ulifikiwa wakati wa Mikutano ya 51 ya Mwaka ya Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB Group) iliyofanyika Baku, Azerbaijan, kuanzia Juni 16 hadi 19 chini ya kaulimbiu ya "Ushirikiano wa Kikanda kwa Ustawi Endelevu."

Fedha hizo zitaelekezwa katika ujenzi wa miundombinu muhimu ya reli ya kilomita 272 kutoka Malaba mpakani mwa Kenya hadi Kampala. Mradi huo unatarajiwa kuwa uti wa mgongo wa mtandao wa reli za kisasa nchini Uganda na kuunganishwa na reli ya Kenya, hivyo kurahisisha usafirishaji wa mizigo kati ya Bandari ya Mombasa na nchi za bara, ikiwemo Uganda.

Kwa mujibu wa Serikali ya Uganda, ufadhili huo utagharamia baadhi ya sehemu muhimu na zenye gharama kubwa zaidi za mradi huo, ikiwemo Daraja la Nile la Jinja lenye urefu wa mita 553, handaki la Mbuya-Kampala lenye urefu wa kilomita 2.12, vituo sita vya reli na karakana tatu za matengenezo.

Hata hivyo, mradi mzima unakadiriwa kugharimu euro bilioni 2.7, hivyo fedha zilizoidhinishwa na IsDB zinawakilisha karibu robo ya gharama zote. Serikali ya Uganda bado inahitaji kutafuta zaidi ya Sh trilioni 8 ili kufikia hatua ya kufunga rasmi mpango mzima wa ufadhili wa mradi huo.

Katika jitihada za kupata sehemu ya fedha zinazohitajika, Uganda ipo katika hatua za mwisho za kuandaa sukuk yake ya kwanza ya taifa yenye thamani ya euro milioni 405 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa reli hiyo. Kwa mujibu wa maafisa wa serikali, sukuk hiyo inatarajiwa kufadhili takribani asilimia 15 ya gharama za mradi, huku asilimia 60 ya fedha zikitarajiwa kutoka taasisi za mikopo ya mauzo ya nje (Export Credit Agencies) na asilimia 25 kutoka taasisi za maendeleo ya kifedha (Development Finance Institutions).



Sukuk hiyo, ambayo inatarajiwa kuzinduliwa katika masoko ya kimataifa mwaka huu, itatolewa kupitia kampuni maalumu ya serikali iitwayo Uganda Treasury Sukuk 1 Limited na kuorodheshwa katika masoko mbalimbali ya fedha duniani ikiwemo Johannesburg Stock Exchange (JSE), Luxembourg Stock Exchange, Nasdaq Dubai, London Stock Exchange na Bursa Malaysia. Serikali ya Uganda inaamini mfumo huo utaisaidia kupata fedha za muda mrefu kwa gharama nafuu zaidi kuliko mikopo ya kawaida inayotegemea riba.

Tofauti na hati fungani za kawaida, sukuk hufuata misingi ya Shariah ambapo wawekezaji hupata mapato yanayotokana na mali au mradi halisi unaowekezwa badala ya riba. Katika muundo wa sukuk ya Uganda, wawekezaji watamiliki sehemu ya miundombinu ya reli huku mapato yao yakitokana na matumizi ya mali hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ya Uganda, Ramathan Ggoobi, ambaye aliongoza ujumbe wa nchi hiyo katika mikutano ya IsDB, alisema serikali inalenga kukamilisha mpango wa ufadhili wa mradi huo ifikapo Novemba mwaka huu.

Mradi huo unatekelezwa na kampuni ya ujenzi ya Uturuki ya Yapi Merkezi, ambayo pia imehusika katika utekelezaji wa sehemu za Reli ya Kisasa ya SGR nchini Tanzania. Serikali ya Uganda inaamini reli hiyo itapunguza gharama za biashara, kuongeza ushindani wa uchumi na kuimarisha biashara ya kikanda wakati nchi za Afrika Mashariki zikiendelea kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya usafiri.

NA UKHTI FATIMA



# Hatua sita za kuanza uwekezaji kwa mafanikio

**Watu wengi wangependa kuwekeza lakini hawajui waanzie wapi. Wengine huamini kuwa uwekezaji ni shughuli ya matajiri pekee, huku wengine wakisubiri hadi wapate mtaji mkubwa kabla ya kuanza. Ukweli ni kwamba safari ya uwekezaji huanza kwa maandalizi sahihi kuliko ukubwa wa fedha ulizonazo. Wataalamu wa fedha wanaeleza kuwa mafanikio katika uwekezaji hayategemei bahati, bali hutokana na nidhamu, maarifa na mipango ya muda mrefu.**

## Jenga msingi imara wa kifedha

Kabla ya kuwekeza, ni muhimu kwanza kuhakikisha hali yako ya kifedha iko katika msingi mzuri.

Moja ya mambo muhimu ni kuwa na akiba ya dharura inayoweza kugharamia matumizi ya miezi mitatu hadi sita iwapo utapoteza kipato au kukumbwa na changamoto zisizotarajiwa.

Pia ni busara kupunguza au kuondoa madeni yanayokuletea mzigo mkubwa wa kifedha. Muislamu anapaswa kuwa mwangalifu na madeni yenye riba na kutafuta njia mbadala zinazokubalika kisheria na kidini.

Aidha, ni muhimu kuwa na bajeti inayokusaidia kujua mapato na matumizi yako kabla ya kufikiria uwekezaji.

## Tambua lengo la uwekezaji

Kila uwekezaji unapaswa kuwa na kusudi maalumu.

Je, unawekeza kwa ajili ya elimu ya watoto? Unajiandaa kwa maisha ya uzeeni? Unakusudia kununua nyumba? Au unataka kuongeza thamani ya mali zako kwa muda mrefu?

Majibu ya maswali haya yatasaidia kuchagua aina ya uwekezaji inayokufaa. Mtu anayejiandaa kwa gharama za miaka 20 ijayo anaweza kuchukua mikakati tofauti na anayehitaji fedha ndani ya miaka miwili au mitatu.

## Jifunze misingi ya uwekezaji

Kabla ya kuweka fedha zako mahali popote, ni muhimu kuelewa kanuni za msingi za uwekezaji.

Miongoni mwa mambo muhimu ni kuelewa uhusiano kati ya faida na hatari. Kwa kawaida, uwekezaji wenye matarajio ya faida kubwa huwa na kiwango kikubwa zaidi cha hatari.

Ni muhimu pia kuelewa dhana ya kugawanya uwekezaji katika maeneo tofauti badala ya kuweka fedha zote sehemu moja. Mbinu hii husaidia kupunguza madhara endapo sekta moja itakumbwa na changamoto.

Kwa Muislamu, hatua hii pia inajumuisha kuhakikisha uwekezaji unaochaguliwa unaendana na misingi ya Sharia na hauhusiani na shughuli zilizokatazwa kama vile riba, kamari au biashara za bidhaa haramu.

## Chagua eneo la kuwekeza

Baada ya kujifunza misingi, hatua inayofuata ni kuchagua sehemu ya kuwekeza.

Baadhi ya watu huwekeza katika biashara zao wenyewe, wengine huwekeza katika hisa za kampuni, mali isiyohamishika kama viwanja na nyumba, au bidhaa za uwekezaji zinazofuata misingi ya fedha za Kiislamu.

Kwa wanaoanza, wataalamu wengi hushauri kuanza na uwekezaji unaoueleweka vizuri badala ya kufuata tu mitindo au ahadi za kupata utajiri wa haraka.

Kumbuka kwamba uwekezaji mzuri ni ule unaoeleweka, unaolindwa na sheria na unaozalisha thamani halisi katika uchumi.

## Kuwa na nidhamu na uthabiti

Moja ya siri kubwa za mafanikio katika uwekezaji ni uthabiti.

Badala ya kusubiri uwe na fedha nyingi sana, unaweza kuanza kwa kiasi kidogo na kuongeza hatua kwa hatua kadiri kipato kinavyokua. Watu wengi waliofanikiwa kifedha walijenga mali zao kwa kuwekeza kiasi kidogo mara kwa mara kwa muda mrefu.

Changamoto nyingine ni kuruhusu hisia kutawala maamuzi. Mara nyingi watu huingiwa na hofu wakati soko linaporudi nyuma au tamaa wakati bei zinapopanda sana. Nidhamu huwasaidia wawekezaji kufanya maamuzi kwa kutumia taarifa sahihi badala ya hisia za muda mfupi.

## Pitia uwekezaji wako mara kwa mara

Uwekezaji si jambo la kufanya mara moja na kulisahau kabisa.

Ni muhimu kuupitia mara kwa mara ili kuona kama bado unaendana na malengo yako. Mahitaji ya maisha hubadilika kadiri miaka inavyopita. Ndoa, watoto, biashara mpya au maandalizi ya kustaafu vinaweza kuhitaji marekebisho ya mpango wako wa uwekezaji.

Pia ni muhimu kuendelea kujifunza kwa sababu mazingira ya biashara na uwekezaji hubadilika kila wakati.

Kwa kuhitimisha, niseme uwekezaji si safari ya siku moja wala si shughuli ya matajiri pekee. Ni mchakato unaohitaji maandalizi, elimu na subira. Kwa kujenga msingi mzuri wa kifedha, kuweka malengo wazi, kujifunza kanuni za uwekezaji na kuchagua fursa zinazokubalika kisheria na kidini, mtu anaweza kujenga ustawi wa kifedha hatua kwa hatua.

Katika Uislamu, mali ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, kuwekeza kwa busara si tu njia ya kutafuta faida, bali pia ni sehemu ya kutumia neema hiyo kwa uwajibikaji na kwa manufaa ya familia na jamii.

## KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Kongole The Islamic Foundation kwa huduma bora za matibabu ya macho

Kuanzia Juni 15 hadi 18, 2026, taasisi ya The Islamic Foundation (TIF) ilitoa huduma za uchunguzi wa macho bila malipo kwa mamia ya wananchi wa mkoa wa Morogoro na kuwafanyia upasuaji wa mtoto wa jicho takriban watu 250.

Huduma hizo zilitolewa na madaktari bingwa wa magonjwa ya macho kutoka Wizara ya Afya, ambao walifanya uchunguzi na tathmini za kitaalamu kwa kila mgonjwa ili kubaini aina ya tatizo na kutoa matibabu stahiki.

Matibabu hayo, yaliyofadhiliwa na shirika la Mercy Outreach Global la Uingereza, yalitolewa katika Kituo cha Al–Jamih for Mother and Child Health Care kilichopo eneo la Msamvu, karibu na Ofisi za Uhamiaji, Morogoro.

Kwa kutambua kuwa macho ni miongoni mwa neema kubwa alizotunukiwa mwanadamu na Allah 'Azza Wajallah', The Islamic Foundation, yenye makao makuu yake Msamvu mkoani Morogoro iliamua kutoa msaada huo kwa wananchi bila kujali umri, jinsia au imani za dini.

Kuwatibu wagonjwa wa macho, kuwapatia vifaa vya kusaidia kuona au kugharamia upasuaji ni kitendo cha huruma kinachorejesha matumaini na kuboresha maisha yao. Haya ni matendo yanayoakisi maadili ya Kiislamu ya kuthamini maisha na utu wa mwanadamu.

Sisi, gazeti la Imaan, tunaipongeza The Islamic Foundation kwa kuwakumbuka na kuwasaidia wagonjwa wa macho, hasa ikizingatiwa kuwa kutatua changamoto za makundi mbalimbali ya jamii ni alama ya hisani mbele ya Mwenyezi Mungu.

Katika Kitabu Kitukufu cha Qur'an, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuambia: "Na saidianeni katika wema na uchamungu, na wala msisaidiane katika dhambi na uadui." [Qur'an, 5:2].

Aya hii inaweka msingi wa mshikamano wa kijamii, ambapo kila mwenye uwezo anapaswa kutumia uwezo wake kuwainua wanaohitaji msaada. Naye Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Atakayemfanyia wepesi mwenye dhiki, Mwenyezi Mungu atamfanyia wepesi duniani na Akhera..." [Muslim].

Pia amesema: "Wenye kurehemu watarehemewa na Mwingi wa rehema. Warehemuni walioko ardhini, atawarehemu aliyeko mbinguni." [Ahmad, Abu Daudi na Tirmidhi]. Hadith hizi mbili zinatukumbusha umuhimu wa kuwasaidia wenye uhitaji ili kuhakikisha wanakuwa katika hali bora ndani ya jamii. Hivyo, tunatoa wito kwa mashirika na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kuendelea kuunga mkono juhudi za utoaji wa huduma za matibabu ya macho, kwa kutambua kwamba kila mchango utakaotolewa ni uwekezaji wa kheri wenye athari chanya duniani na Akhera.



MAKALA ZA WAQF

NA IDARA YA ELIMU, AWQAF TANZANIA

# Haja na hoja ya benki ya ardhi: Fursa ya dhahabu kwa vizazi vijavyo kupitia urithi wa waqf

**Katika kipindi hiki cha mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii, rasilimali inayozidi kuwa ya thamani duniani si fedha pekee bali pia ardhi.**

**Kadri idadi ya watu inavyoongezeka na mahitaji ya makazi, kilimo na uwekezaji yanavyopanuka, umiliki wa ardhi unazidi kuwa msingi muhimu wa ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.**

**Katika muktadha huo, wito uliotolewa hivi karibuni na Mufti Sheikh Abubakar Zubeir kupitia Tamko la Madina kuhusu umuhimu wa Waislamu kumiliki na kuhifadhi ardhi kwa manufaa ya baadae ni wa muhimu sana.**

**Wito huo unahamasisha Waumini kununua ardhi, kuitunza na kuifikiria kama mali inayoweza kutolewa waqf au kuendelezwa kwa manufaa ya jamii.**

## Ardhi kama benki ya uwekezaji wa vizazi

Duniani kote, ardhi imeendelea kuwa mojawapo ya mali salama zaidi za uwekezaji wa muda mrefu. Tofauti na fedha zinazoweza kuathiriwa na mfumuko wa bei au mali zinazochakaa, ardhi mara nyingi huongezeka thamani kadiri muda unavyopita.

Kwa mtazamo huo, dhana ya "Benki ya Ardhi" ni mkakati wa kuweka akiba ya rasilimali kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Kumiliki ardhi leo si suala la kutafuta faida ya haraka pekee, bali ni uwekezaji unaoweza kuwa msingi wa makazi, kilimo, biashara na shughuli nyingine za kiuchumi kwa watoto na wajukuu wetu.

## Waqf, chombo cha maendeleo endelevu

Historia ya Uislamu inaonesha kuwa mfumo wa waqf umekuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya jamii. Kupitia waqf, ardhi na mali nyingine zimewezesha ujenzi wa misikiti, shule, vyuo, hospitali na taasisi mbalimbali za huduma za kijamii.

Faida kubwa ya waqf ni kwamba manufaa yake huendelea kwa muda mrefu. Mapato yatokanayo na mali za waqf yanaweza kusaidia kugharamia elimu, afya na huduma nyingine za kijamii kwa vizazi vingi. Hivyo, waqf si ibada pekee, bali pia nyenzo ya kujenga uchumi imara wa kijamii.

## Kuepuka changamoto za urithi wa mali

Katika jamii nyingi, wazazi hujitahidi kuacha majengo, fedha na mali nyingine kwa ajili ya watoto wao. Hata hivyo, mali hizo wakati mwingine hukumbwa na migogoro ya urithi au hupotea kutokana na usimamizi dhaifu.

Ardhi iliyowekwa waqf inaweza kuwa njia ya kuhifadhi rasilimali kwa muda mrefu. Mfumo huu husaidia kuhakikisha kuwa mali hiyo inaendelea kutumika kwa manufaa ya jamii badala ya kugawanywa au kuuzwa bila mpango. Kwa maana hiyo, waqf hauachi mali pekee, bali huacha mfumo endelevu wa kuzalisha manufaa.

## Wito kwa Waislamu na wawekezaji

Ili kufanikisha maono ya kuwa na Benki ya Ardhi kwa manufaa ya vizazi vijavyo, kuna mambo matatu ya kuzingatia.

Kwanza, kununua ardhi kadri uwezo unavyoruhusu, hata kama ni eneo dogo. Pili, kuitunza kwa mtazamo wa muda mrefu badala ya kutafuta faida ya haraka. Ardhi inaweza kuendelezwa kupitia upandaji miti, kilimo au miradi mingine ya maendeleo.

Tatu, kutenga sehemu ya ardhi kwa ajili ya waqf na kuhakikisha inasimamiwa na watu au taasisi zenye uadilifu na uwezo wa kusimamia mali hizo kwa manufaa yaliyokusudiwa. Aidha, ni muhimu waqf kusajiliwa kwa mujibu wa sheria ili kulinda dhamira ya mtoaji.

## Msingi wa Kiislamu wa uwekezaji wa Waqf

Mafundisho ya Kiislamu yanahimiza matumizi ya mali kwa manufaa ya jamii na uwekezaji wa muda mrefu. Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an, [2: 261]: "Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje iliyotoa masuke saba, katika kila suke zikiwa punje mia moja; na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye."

Aya hii inaonesha kuwa matumizi ya mali kwa manufaa ya watu yanaweza kuzaa matunda makubwa kuliko thamani yake ya awali. Ardhi inayowekwa waqf na kuendelezwa kwa manufaa ya jamii inaweza kuwa mfano halisi wa uwekezaji huo.

Vilevile, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alisisitiza umuhimu wa sadaka yenye manufaa ya kudumu. Katika muktadha wa waqf. Ardhi inayotumika kujenga shule, hospitali, misikiti au miradi mingine ya kijamii inaweza kuendelea kuwanufaisha watu hata baada ya mtoaji kufariki dunia.

## Hitimisho

Wazo la Benki ya Ardhi si suala la umiliki wa ardhi pekee, bali ni mkakati wa kujenga mustakabali wa vizazi vijavyo. Kupitia umiliki wa ardhi, uwekezaji wa muda mrefu na matumizi ya mfumo wa waqf, jamii inaweza kujenga msingi imara wa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiroho.

Ni wakati wa kufikiri zaidi ya mahitaji ya leo na kuwekeza katika rasilimali zitakazobaki kuwa nguzo ya ustawi wa watoto, wajukuu na vizazi vijavyo.

مُحرم

TAFAKURI YA MWAKA MPYA 1448



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Hijra katika Qur'an na Sunnah: Safari ya imani na mabadiliko

**Hijra ni miongoni mwa dhana muhimu katika Uislamu. Watu wengi wanapoitaja hijra, hukumbuka kuhama kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) na Swahaba zake kutoka Makka kwenda Madina. Hata hivyo, Qur'an na Sunna zinaonesha kuwa hijra ni dhana pana zaidi inayohusisha kulinda dini, kutafuta usalama, kuondoka kwenye dhulma, na hata kujiepusha na maasi. Katika historia ya Mitume, hijra imekuwa njia ya kuhifadhi ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kujenga jamii zenye msingi wa haki na uongofu. Kwa sababu hiyo, hijra si tukio la kihistoria pekee, bali ni sehemu ya maisha ya waumini katika nyakati zote.**

## Maana ya Hijra katika Uislamu

Kwa maana ya kisheria, hijra ni kuhama kutoka sehemu ambayo mtu hawezi kutekeleza dini yake kwa uhuru au kuihifadhi ipasavyo kwenda sehemu yenye usalama na mazingira bora zaidi ya kuishi kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an Tukufu inasema: "Je, ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa pana mkahama humo?" [Quran, 4: 97].

Aya hii inaonesha kwamba pale ambapo mtu ana uwezo wa kuhama ili kulinda dini yake na kujinasua kutoka katika hali ya kudhulumiwa, basi hijra huwa njia halali na yenye umuhimu mkubwa.

Sunna nayo imepanua maana ya hijra zaidi ya kuhama kimwili. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Muhajiri ni yule anayoyaacha mambo aliyoyakataza Mwenyezi Mungu." Hadith hii inatufundisha kuwa hijra pia ni kuacha maovu, dhambi na tabia mbaya, na kuelekea kwenye utiifu wa Mwenyezi Mungu.

## Hijra ni Sunna ya Mitume

Qur'an inaonesha wazi kuwa hijra haikuanza kwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani). Mitume wengi waliitangulia katika njia hiyo.

Nabii Ibrahim (Allah amshushie amani) alisema: "Hakika mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima." [Qur'an, 29: 26].

Nabii Musa (Allah amshushie amani) naye alilazimika kuondoka Misri kutokana na vitisho vya Firauni. Qur'an inasema: "Akatoka humo akiwa na hofu na akitazama huku na huku." [Qur'an, 28: 21]. Vilevile, wana wa Israil walitoka Misri kwa amri ya Mwenyezi Mungu wakiongozwa na Nabii Musa (Allah amshushie amani), jambo linaloonesha kuwa hijra ilikuwa njia ya kuokoa imani na maisha ya Waumini.

## Sababu zinazowafanya watu kuhama

Miongoni mwa sababu zilizotajwa katika Qur'an na Sunna ni kulinda dini na imani. Waumini wa mwanzo walihama ili waweze kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa uhuru bila mateso wala vikwazo.

Sababu nyingine ni kukimbia dhulma na ukandamizaji. Qur'an imezungumzia watu waliokuwa wakiteswa kwa sababu ya imani zao na ikawahimiza kutafuta sehemu salama ikiwa wana uwezo wa kufanya hivyo. Pia, kutafuta usalama ni sababu halali ya kuhama. Hili linaonekana katika kisa cha Nabii Musa (Allah amshushie amani.) alipoondoka kwa hofu ya kuuawa.

Kwa upande mwingine, mazingira ya maisha yanaweza kuwa sababu ya kuhama. Historia ya Nabii Yusuf (Allah amshushie amani) inaonesha jinsi njaa na ukame vilivyosababisha watu kuhama kwenda kutafuta riziki na maisha bora.

## Aina za Hijra

Qur'an imeonesha aina mbalimbali za hijra. Kuna hijra ya mtu mmoja mmoja, kama ilivyokuwa kwa Ibrahim na Musa (Allah awashushie amani) na kuna hijra ya kifamilia, ambapo mtu huhama pamoja na familia yake kwa ajili ya usalama au maisha bora.

Pia kuna hijra ya kijamii au ya kundi kubwa la watu, kama ilivyokuwa kwa wana wa Israil walipotoka Misri na kwa Waislamu walipohama kutoka Makka kwenda Madina.

Zaidi ya hayo, kuna hijra ya kiroho na kimaadili, ambayo ni kuacha maasi na kuanza maisha ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu.

## Sifa za wahajiri na malipo yao

Qur'an imewasifu wahajiri kwa sifa nyingi nzuri. Miongoni mwa sifa hizo ni imani, subira, kujitolea na kuwa tayari kuvumilia matatizo kwa ajili ya dini. Wahajiri wa mwanzo walikubali kuacha nyumba zao, mali zao na mazingira waliyozoea kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo, Qur'an imewataja kwa heshima kubwa na kuwapa bishara ya malipo makubwa duniani na Akhera.

Mwenyezi Mungu amewaahidi wahajiri malipo makubwa. Qur'an inataja kwamba wale waliohama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu watapata riziki njema, msamaha wa dhambi na daraja kubwa mbele ya Mola wao Mlezi.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) pia alibainisha kwamba baada ya kufunguliwa Makka hakukuwa tena na ulazima wa kuhama kutoka Makka kwenda Madina, lakini kanuni ya hijra yenye sababu zake halali iliendelea kuwepo. Nihitimishe kwa kusema kuwa mafundisho ya Qur'an na Sunna yanaonesha kuwa hijra ni zaidi ya kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Ni safari ya kulinda imani, kutafuta usalama, kujiepusha na dhulma na kujenga maisha bora.

Aidha, hijra ina maana ya ndani inayomhusu kila Muislamu, nayo ni kuacha maovu na kuelekea kwenye utiifu wa Mwenyezi Mungu. Hivyo, hijra ni mchakato endelevu wa mabadiliko na marekebisho ya maisha, unaomsaidia mwanadamu kutimiza wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu na kwa jamii inayomzunguka.




UCHAMBUZI MAALUM

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Utitiri wa taasisi za Kiislamu uwe na tija kwa umma wa Kiislamu

**Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko kubwa la taasisi mbalimbali za Kiislamu nchini Tanzania. Taasisi hizi zimeanzishwa kwa malengo tofauti yakiwemo kueneza elimu ya dini, kusaidia jamii, kuimarisha maadili na kuchangia maendeleo ya Waislamu kwa ujumla. Kwa hakika, hatua hii ni ya kupongezwa kwa sababu inaonesha mwamko mpya miongoni mwa Waislamu wa Tanzania wa kutafuta suluhisho la changamoto zinazoukabili umma wao.**

**Ni jambo la kutia moyo kuona vijana, wasomi, wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa Kiislamu wakijitolea muda, rasilimali na maarifa yao kuanzisha taasisi zinazolenga kuhudumia jamii.**

**Hii ni ishara kwamba Waislamu hawajakaa kimya bali wanatafuta njia za kujenga mustakabali bora wa umma wao. Kila taasisi inayozaliwa ikiwa na nia njema ya kutumikia dini na jamii inastahili kutiwa moyo na kuungwa mkono.**

## Mwelekeo mpya

Hata hivyo, pamoja na kupongeza juhudi hizi, kuna haja ya kutafakari kwa kina kuhusu mwelekeo wa taasisi hizi na matokeo yake kwa jamii pana ya Kiislam. Swali la msingi siyo idadi ya taasisi zilizopo, bali ni athari zake kwa umma. Tunaweza kuwa na taasisi nyingi sana lakini zisizoleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Waislam.

Vivyo hivyo, tunaweza kuwa na taasisi chache lakini zenye mchango mkubwa unaogusa maisha ya watu kwa upana zaidi.

Changamoto inayojitokeza mara nyingi ni kuona taasisi nyingi zikifanya shughuli zinazofanana.

Mara nyingi taasisi mpya zinapoanzishwa hukimbilia kuandaa mashindano ya Qur'an, mihadhara ya dini au kuchangia ujenzi wa misikiti. Hakuna ubaya katika shughuli hizi, kwani zote zina nafasi muhimu katika kuimarisha dini.

Hata hivyo, tatizo linatokea pale ambapo karibu kila taasisi inajikita katika eneo hilo hilo huku maeneo mengine muhimu yakiachwa bila huduma za kutosha.

Leo hii, umma wa Kiislamu unakabiliwa na changamoto nyingi zaidi ya zile zinazohitaji majibu ya kiibada pekee. Kuna changamoto za kiuchumi, kielimu, kiafya, kijamii na kiteknolojia. Kuna vijana wengi wasio na ajira, familia zinazopambana na umasikini, watoto wanaokosa elimu bora na jamii zinazokabiliwa na mmomonyoko wa maadili kutokana na mazingira yanayowazunguka.

Haya yote yanahitaji taasisi zenye fikra mpya na mbinu bunifu za kuyashughulikia.

Ni wakati sasa kwa taasisi za Kiislamu kuanza kujiuliza ni pengo gani ambalo halijazibwa katika jamii. Badala ya kuiga kile kinachofanywa na wengine, taasisi zifikirie namna ya kuleta thamani mpya. Tunaweza kuwa na taasisi zinazojikita katika uwezeshaji wa kiuchumi kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, mikopo isiyo na riba kwa vijana na wanawake, au miradi ya kilimo na ufugaji inayowawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi.

## Twendeni vijijini

Vilevile, kuna haja ya kuona taasisi nyingi zaidi zikielekeza nguvu zao vijijini. Ukweli ni kwamba wapo Waislamu wanaoishi katika maeneo ya vijijini ambako changamoto za maendeleo ni kubwa zaidi.

Mara nyingi shughuli nyingi za taasisi huonekana katika miji mikubwa wakati vijiji vikibaki nyuma. Taasisi za Kiislamu zinapaswa kuwa mstari wa mbele kufikisha huduma za elimu, afya, maji safi, mafunzo ya ufundi na miradi ya uzalishaji katika maeneo hayo.

Aidha, taasisi zinaweza kuanzisha vituo vya mafunzo ya stadi za maisha, programu za kuwawezesha vijana kutumia teknolojia, au kampeni za kupambana na changamoto za kijamii kama matumizi ya dawa za kulevya, migogoro ya kifamilia na ukatili wa kijinsia.

Haya ni maeneo ambayo yanahitaji nguvu kubwa za kijamii na yanaweza kuleta mabadiliko ya kudumu katika maisha ya wananchi.

Jambo jingine muhimu ni ushirikiano. Badala ya kila taasisi kufanya kazi kivyake, kuna umuhimu wa kujenga utamaduni wa kushirikiana na kugawana uzoefu. Taasisi zikifanya kazi kwa pamoja zinaweza kufikia watu wengi zaidi, kutumia rasilimali kwa ufanisi na kuepuka kurudia shughuli zilezile katika eneo moja huku maeneo mengine yakisahaulika.

Kwa hakika, umma wa Kiislamu wa Tanzania una kila sababu ya kufurahia mwamko wa kuanzishwa kwa taasisi nyingi za Kiislamu.

Huu ni mtaji mkubwa ambao ukitumiwa vizuri unaweza kuleta mapinduzi makubwa ya maendeleo. Hata hivyo, mafanikio ya taasisi hizi hayatapimwa kwa idadi ya semina, mashindano au majengo yaliyojengwa pekee, bali kwa kiwango cha mabadiliko yatakayopatikana katika maisha ya Waislamu na jamii kwa ujumla.

Tunachohitaji leo ni taasisi zenye maono mapana, ubunifu mkubwa na uwezo wa kugusa changamoto halisi za wananchi. Tunahitaji taasisi zinazojenga uchumi wa Waislam, zinazowekeza kwa vijana, zinazofika vijijini, zinazotatua matatizo ya kijamii na zinazoweka msingi wa maendeleo endelevu. Hapo ndipo utitiri wa taasisi utakapokuwa na maana ya kweli, na hapo ndipo umma wa Kiislamu utaanza kunufaika kikamilifu na nguvu ya taasisi zake.

Kwa hiyo, wakati tunapongeza juhudi zote za kuanzisha taasisi za Kiislamu nchini Tanzania, tunapaswa pia kusisitiza kuwa taasisi hizo ziwe na tija, ubunifu na athari chanya kwa umma. Idadi ni muhimu, lakini matokeo ndiyo kipimo halisi cha mafanikio.

مُحرم

فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Hukumu ya kusherehekea siku ya kuzaliwa

**Swali:** **Ni ipi hukumu ya kuadhimisha siku za kuzaliwa kwa mtu au watoto (birth day) au kufanya sherehe ya kumbukumbu ya ndoa?**

**Jibu:** Katika Uislamu hakuna sikukuu nyingine isipokuwa Ijumaa ambayo ni sikukuu ya kila wiki, siku ya kwanza ya mwezi wa Shawwal ambayo ni Sikukuu ya Eid el Fitr baada ya Ramadhan na siku ya kumi ya mwezi wa Dhul-Hijjah ambayo ni Sikukuu ya Eid el Adh-haa.

Siku ya Arafa pia inaweza kuitwa sikukuu kwa watu walioko Arafa , na siku za Tashriq ni siku za sikukuu zinazofuatia Eid el Adh-ha.

Ama sikukuu za kuzaliwa kwa mtu au watoto wake, au sherehe za kumbukumbu ya ndoa na mfano wake, zote si za kisheria (hazikupendekezwa katika dini), na ziko karibu zaidi na uzushi (bid'ah) kuliko kuwa jambo linaloruhusiwa. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali:** **Kuna mzazi anamziwia mwanawe wa kiume kwenda kuoa mwananmke wa kutoka Mkoa fulani na anasema: akioa huko hatamtambua mkwewe, hili likoje kidini?**

**Jibu:** Katika Uislamu, mzazi ana haki kubwa sana ya kuheshimiwa na kutiiwa, lakini utiifu huo una mipaka. Ikiwa mzazi anamkataza mwanawe kuoa mwanamke mwema kwa sababu zisizo za Kisharia, kama vile tu kwa sababu anatoka Mkoa fulani, Kabila fulani, au familia fulani bila sababu ya dini au maadili, basi katazo hilo halimlazimu mwana kutekeleza.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna utiifu kwa kiumbe katika kumuasi Muumba." [Ahmad].

Wanazuoni wameeleza kuwa ikiwa mwanamke ana dini na tabia njema, basi haifai kumzuia mtu kumuoa kwa sababu za kibaguzi au chuki zisizo na msingi wa Kisharia.

Hata hivyo, mwana anatakiwa: Aendelee kumheshimu mzazi wake. Azungumze naye kwa upole na hekima. Ajitahidi kumridhisha na kumuondolea wasiwasi wake. Aepuke ugomvi na kukata uhusiano.

Ama kauli ya mzazi kusema: "Ukioa huko sitamtambua huyo mkeo," kauli hiyo haina athari katika uhalali wa ndoa. Ikiwa ndoa imetimia kwa masharti yake ya Kisharia, mke huyo ni mke halali, na mzazi anapaswa kutunza haki za udugu na ukwe bila dhulma.

Lakini kama mzazi ana sababu za msingi za Kisharia —kwa mfano anajua mwanamke huyo ana tabia mbaya, upotovu wa dini, au kuna madhara ya wazi yatakayotokana na ndoa hiyo— basi ni muhimu mwana kuyazingatia mashauri yake kwa uzito mkubwa.

Kwa hiyo, ikiwa sababu ni kwamba tu mwanamke anatoka Mkoa fulani, basi hilo si sababu ya Kisharia ya kuzuia ndoa, wala si halali kumdharau au kutomtambua mkwe kwa msingi huo. Allah amesema: "Hakika aliye mtukufu zaidi kwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye mchamungu zaidi miongoni mwenu." [Qur'an, 49:13].

Zaidi Kigezo katika Uislamu ni dini, uchamungu na maadili mema, si mkoa, kabila au nasaba pekee. Na Allah ndiye Mjuzi




MAKALA MAALUM

MAHMOUD NYAMGUMA

# Uhamaji wa kiteknolojia, kiutamaduni katika mwaka mpya wa Kiislamu

Kuingia kwa Mwaka Mpya wa Hijria wa 1448 si tukio la kubadili kalenda au kutumiana jumbe za baraka, hasa zama hizi ambapo umma wa Kiislamu umesimama kwenye njia panda ya kihistoria.

Huu ni muda ambapo umma unatakiwa kufanya Hijrah (uhamiaji) mpya, sio wa kijiografia, kutoka mji mmoja kwenda mwingine, bali uhamiaji wa kifikra, kiteknolojia na kiutamaduni.

Kwanza, nikitazama upande wa siasa za kijiografia (geopolitics), inasikitisha kuona jinsi ulimwengu wa Kiislamu unavyomiliki maeneo muhimu zaidi ya kimkakati na rasilimali nyingi za dunia, lakini bado umekosa sauti moja yenye nguvu.

Mitandao imejaa ripoti za migogoro isiyoisha na utegemezi mkubwa wa kiusalama kutoka kwa mataifa ya Magharibi na Mashariki. Ukweli ni kuwa, hadi pale mataifa ya Kiislamu yatakapoacha kuweka mbele maslahi ya kisiasa ya muda mfupi na kujenga diplomasia huru ya pamoja; basi utajiri wa rasilimali utabaki kuwa laana badala ya kuwa baraka.

Mwaka 1448 unatazamwa kama mwanzo wa kuunda mifumo thabiti ya kiusalama na kiuchumi ya ndani inayoweza kutatua migogoro ya kieneo bila kusubiri maelekezo kutoka miji mikuu ya Magharibi au Mashariki ya Mbali.

Pili, tunapoangalia ripoti za maendeleo ya Akili Mnemba (AI) na Sayansi ya Data (Big Data), ulimwengu wa Kiislamu bado upo nyuma kwenye nafasi ya ugunduzi, huku ukiwa mstari wa mbele kama mtumiaji mkuu (consumer). Hata hivyo, teknolojia ndio inaamua nani atatawala kesho.

Kama mifumo ya AI inaundwa na algorithms zisizojali maadili au utamaduni wa Kiislamu, tunakaribisha ukoloni mamboleo wa kidijitali. Umma unahitaji kuwekeza kwa nguvu zote kwenye elimu ya STEM ili kutengeneza 'Teknolojia yenye maadili' (Ethical Tech) itakayolinda misingi ya jamii badala ya kuibomoa.

Tatu, kwenye upande wa maadili na maisha ya sasa (modern living), kuna vita vya kimya kimya vinavyoendelea kwenye mitandao ya kijamii ambavyo vinalenga kutengeneza utambulisho mpya wa mwanadamu usio na mipaka ya kidini wala kitamaduni.

Hili linatikisa msingi wa familia, ambayo ndiyo nguzo ya jamii yoyote. Hata hivyo, suluhu sio kukimbia mitandao au kujifungia ndani. Maoni yangu ni kwamba, tunapaswa kutumia dhana ya Wasatiyyah (msimamo wa wastani) kama dira ya kisasa.

Waislamu wanapaswa kuwa vinara wa kuonyesha kuwa unaweza kuwa mwanasayansi mahiri, mfanyabiashara mkubwa wa kidijitali, au kiongozi wa kisasa, huku ukiwa na uaminifu usiotikisika, ukipinga rushwa, na ukilinda heshima ya kifamilia.

Mwisho kabisa, ninaiyona sekta ya uchumi wa Kiislamu (Islamic Finance) na uchumi wa kijani (Green Economy) kama fursa kubwa zaidi ambayo bado haijatumiwa ipasavyo. Mafundisho ya Kiislamu kuhusu utunzaji wa mazingira kama dhamana (Khalifah) na ukatazwaji wa riba yanatoa suluhu ya moja kwa moja kwa migogoro ya sasa ya kiuchumi duniani na mabadiliko ya tabianchi.

Kuelekea 1448 Hijria, umma lazima uongoze kwa mfano katika kilimo endelevu, nishati safi, na mifumo ya kifedha inayojali utu na usawa.

Umma wa Kiislamu usitazame mwaka huu kama mwanzo wa karne tu, bali uutazame kama saa ya kengele inayotutaka tuamke kutoka kwenye usingizi wa kifikra na kuchukua nafasi yetu stahiki ya kuongoza ulimwengu kwa uadilifu, amani, na ustawi.





# Watoto chini ya miaka 15 marufuku kutumia mitandao ya Kijamii UAE

***ABU DHABI*** — Falme za Kiarabu (UAE) imepitisha sheria mpya inayowazuia watoto walio chini ya umri wa miaka 15 kutumia mitandao ya kijamii, hatua inayolenga kuwalinda dhidi ya hatari za mazingira ya kidijitali na kuifanya nchi hiyo kuwa ya kwanza katika ulimwengu wa Kiarabu kuweka kizuizi hicho.

Kwa mujibu wa azimio lililoidhinishwa na Baraza la Mawaziri, watoto chini ya miaka 15 hawataruhusiwa kufungua, kutumia au kuendesha akaunti binafsi katika majukwaa ya mitandao ya kijamii. Pia hawataruhusiwa kuchapisha maudhui, kutoa maoni, kushiriki taarifa au kujiunga na makundi ya umma.

Watoto wenye umri wa miaka 15 na 16 wataruhusiwa kutumia mitandao hiyo chini ya masharti maalumu, ikiwemo mifumo ya kudhibiti muda wa matumizi, maudhui yanayolingana na umri wao, udhibiti wa wazazi na vikwazo vya mawasiliano na watu wasiowafahamu.

Serikali ya UAE imeipa kampuni za mitandao ya kijamii kipindi cha hadi miezi 12 kutekeleza masharti hayo na kuweka mifumo madhubuti ya kuthibitisha umri wa watumiaji. Kampuni zitakazoshindwa kutii zinaweza kupewa onyo, kutozwa adhabu au hata kuzuiwa kutoa huduma nchini humo.

Aidha, sheria hiyo inapiga marufuku matumizi ya taarifa binafsi za watoto kwa madhumuni ya kibiashara au matangazo yanayotokana na kufuatilia shughuli zao mtandaoni.

Hatua hiyo imekuja wakati mataifa mbalimbali duniani yakiongeza juhudi za kuwalinda watoto dhidi ya maudhui yasiyofaa, matumizi kupita kiasi ya mitandao ya kijamii, unyanyasaji wa mtandaoni na ukusanyaji wa taarifa zao binafsi bila ulinzi wa kutosha.

# Nchi saba zailaumu Israel kwa mashambulizi ya misikiti Ukingo wa Magharibi

***RIYADH*** — Mawaziri wa Mambo ya Nje wa nchi nane zenye Waislamu wengi, zikiwemo Saudi Arabia, Uturuki, Jordan, Qatar, Misri, Falme za Kiarabu (UAE), Indonesia na Pakistan, wameishutumu Israel na kuitaka iwajibike kwa matukio ya uchomaji moto misikiti miwili katika eneo la Ukingo wa Magharibi (West Bank).

Kwa mujibu wa The New Arab, eneo hilo linakaliwa kwa mabavu na Israel na viongozi wa Kipalestina wanasema mashambulizi hayo yalifanywa na walowezi wa Kiyahudi.

Katika taarifa ya pamoja iliyotolewa Alhamisi, mawaziri hao walilaani kuongezeka kwa vitendo vya vurugu dhidi ya Wapalestina na kueleza kuwa Israel, kama mamlaka inayoshikilia eneo hilo kwa mabavu, inapaswa kubeba dhamana ya kulinda maeneo matakatifu na raia walioko chini ya mamlaka yake. Taarifa hiyo ilitolewa siku moja baada ya misikiti katika vijiji vya Jiljiliya na Mazari an-Nubani, kaskazini mwa Ramallah, kuripotiwa kuchomwa moto. Mameya wa vijiji hivyo walisema walowezi walivamia maeneo hayo na kushambulia na kuharibu misikiti.




MAKALA MAALUM

UKHTI FATMA SS

# Mwaka mpya wa Kiislamu 1448: Ni ipi Hijra yako mwaka huu?

Waislamu duniani kote wameupokea mwaka mpya wa Kiislamu 1448 Hijria kwa kuanza kwa mwezi wa Muharram, mwezi wa kwanza katika kalenda ya Kiislamu. Hata hivyo, tofauti na namna mataifa mengi duniani yanavyoadhimisha kuanza kwa mwaka mpya kwa sherehe, fataki na tafrija, mwaka mpya wa Kiislamu huja na ujumbe tofauti: ujumbe wa muhaseba, tafakuri na mabadiliko.

Kalenda ya Hijria hutegemea mzunguko wa mwezi, hivyo mwaka wake huwa na siku 354 au 355, chini ya kalenda ya Gregori kwa takribani siku 11. Lakini umuhimu wa mwaka mpya wa Kiislamu hauko katika tofauti za kihisabati za kalenda. Umuhimu wake uko katika historia na mafunzo yaliyozaa mwanzo wa kalenda hiyo.

Asili ya kalenda ya Hijria inatokana na tukio la Hijra — uhamaji wa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kutoka Makka kwenda Madina mwaka 622 Miladia. Uhamaji huo haukuwa safari ya kawaida ya kutoka mji mmoja kwenda mwingine. Ulikuwa hatua ya kihistoria iliyobadilisha mwelekeo wa Uislamu na kuanzisha jamii mpya iliyojengwa juu ya misingi ya imani, haki, udugu na uwajibikaji.

## Hijra, mwanzo wa kalenda

Ndiyo maana katika ukhalifa wa Umar bin Al-Khattab (Allah amridhie), Waislamu walipoamua kuanzisha mfumo rasmi wa kuhesabu miaka, walichagua Hijra kuwa mwanzo wa kalenda yao. Uamuzi huo ulikuwa na ujumbe mkubwa. Haukuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume, ushindi wa vita au mafanikio ya kiuchumi. Uliadhimisha kujitolea kwa ajili ya ukweli, subira katika mitihani na ujenzi wa jamii bora.

Mwezi wa Muharram unaoanzisha mwaka mpya wa Hijria ni miongoni mwa miezi minne mitukufu iliyotajwa katika Qur'an. Ndani ya mwezi huu, Waislamu wanahimizwa kuongeza ibada, kutenda mema na kujiepusha zaidi na maasi. Ni mwezi unaomkumbusha mja kurekebisha uhusiano wake na Mwenyezi Mungu na kutafakari mwenendo wa maisha yake.

Muharram pia hubeba kumbukumbu muhimu katika historia ya Mitume. Siku ya Ashura, ambayo ni tarehe 10 Muharram, ina nafasi ya pekee katika Uislamu. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alifunga siku hiyo kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumuokoa Nabii Musa (Amani ya Allah imshukie) na wana wa Israil dhidi ya Fira'un. Aidha, aliwahimiza Waislamu kufunga siku hiyo, akieleza kuwa kufunga Ashura kwa ikhlasi ni sababu ya kusamehewa madhambi madogo ya mwaka uliotangulia.

Hata hivyo, mafunzo makubwa ya Muharram hayaishii katika historia wala ibada za mwezi huu pekee. Kiini cha Hijra ni mabadiliko. Ni safari kutoka hali moja kwenda hali bora zaidi.

## Ni ipi Hijra yako mwaka huu?

Hapa ndipo mwaka mpya wa Kiislamu unapopata maana halisi katika maisha ya kila Mwislamu. Kama Hijra ilikuwa kuhama kutoka mazingira ya dhuluma kwenda mazingira ya haki, kutoka udhaifu kwenda nguvu, na kutoka mateso kwenda matumaini, basi kila mmoja wetu anapaswa kujiuliza: Hijra yangu mwaka huu ni ipi?

Je, ni Hijra kutoka uzembe kwenda uwajibikaji? Kutoka migogoro kwenda maridhiano? Kutoka matumizi mabaya ya muda kwenda uzalishaji? Kutoka chuki kwenda msamaha? Kutoka dhambi kwenda utiifu wa Mwenyezi Mungu?

Maswali hayo ni muhimu zaidi kuliko kubadilika kwa tarehe kwenye kalenda.

Katika zama hizi zinazoshuhudia migogoro ya kijamii, changamoto za kiuchumi, mmomonyoko wa maadili na kuongezeka kwa mgawanyiko wa watu, historia ya Hijra inatukumbusha kuwa mabadiliko makubwa ya jamii huanza na mabadiliko ya mtu mmoja mmoja. Madina haikujengwa kwa majengo makubwa kwanza; ilijengwa kwa watu waliobadilika fikra, tabia na mtazamo wao wa maisha.

Hivyo basi, mwaka mpya wa 1448 Hijria unapaswa kuwa zaidi ya salamu za heri na ujumbe wa pongezi. Ni fursa ya kufanya muhaseba wa kina kuhusu tulikotoka na tunakotaka kwenda. Ni wakati wa kuomba msamaha kwa makosa yaliyopita, kurekebisha mahusiano yaliyovunjika, kuimarisha ibada na kuweka malengo mapya ya kiroho, kijamii na kimaadili.

Kwa hakika, maana ya mwaka mpya wa Kiislamu si kubadilika kwa namba ya mwaka, bali kubadilika kwa maisha. Na kama historia ya Hijra inavyotufundisha, mabadiliko ya Umma huanza pale mtu mmoja anapoamua kuanza Hijra mpya ndani ya nafsi yake.



**MAKALA MAALUM**

**SEHEMU YA 2**

Na Said Rajab
0783 650 803



# VITA MASHARIKI YA KATI:

# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulimaliza kwa kusema kwamba wapatanishi halisi katika siasa za kimataifa wana ushawishi juu ya pande zote mbili zinazokinzana – uwe wa kijeshi, kiuchumi, kisiasa, au kidiplomasia.

# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulimaliza kwa kusema kwamba wapatanishi halisi katika siasa za kimataifa wana ushawishi juu ya pande zote mbili zinazokinzana – uwe wa kijeshi, kiuchumi, kisiasa, au kidiplomasia.

Tulieleza kuwa Pakistan haina chochote kati ya hivyo. Badala ya kutegemea ushawishi wake wa kidiplomasia, inategemea nguvu na msaada wa wengine katika kusukuma mbele maslahi yake.

Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho tutalinganisha hali hiyo na kile ambacho Pakistan inafanya kwa sasa. Sasa endelea...

Pakistan inaandaa mikutano na kutoa miito, inashirikisha nchi nyingine za Waislamu, inafanya kazi kama daraja la mawasiliano, inapitisha ujumbe kati ya pande hizo mbili, inafanya kazi ndani ya juhudi pana za kidiplomasia zilizoratibiwa, inasafiri kati ya miji mikuu ya China, Saudi Arabia, Uturuki, Qatar na Misri ili kutafuta upatanishi, mwelekeo na usaidizi.

Swali linakuja, uko wapi umahiri wa Pakistan kama dola? Kwa hakika, hii siyo Pakistan inayoongoza juhudi za usuluhishi wa mgogoro wa Marekani na Iran.

Baadhi ya wachambuzi wameeleza jukumu la Pakistan kama mwezeshaji, tarishi, na njia ya mawasiliano ya Marekani kwa niaba ya Wamarekani. Hii ni kazi ambayo hakuna mtu mwingine anayeitaka.

Hii hapa nukta ya msingi. Majukumu kama haya huwa hayajitokezi tu. Katika siasa za kisasa za kijiografia (geopolitics), mataifa makubwa hutoa idhini yao kimya kimya na hufanya kazi kupitia wapatanishi na matarishi kama hawa.

Kwa hiyo, swali halisi ni nani anayeweka ajenda kwa Pakistan? Ni wazi siyo Pakistan. Kwanini Pakistan? Pakistan siyo nchi ya kwanza kubeba jukumu hili, tumeona nchi nyingine kadhaa zikifanya hivyo ikiwamo Qatar, Uturuki, Saudi Arabia, na hivi karibuni Oman.

Mara nyingi nchi hizi zimekuwa zikiingilia migogoro ya mataifa mengine kama wawezeshaji, njia ya mawasiliano, au matarishi, kwa amri ya Wamarekani, ndani ya mfumo mpana zaidi wa kidiplomasia unaoongozwa na Marekani.

Angalia jinsi mwelekeo wa diplomasia ya kikanda unavyojitokeza. Uturuki imejijengea nafasi muhimu kama mpatanishi katika mazungumzo kati ya Urusi na Ukraine. Oman imekuwa kiungo muhimu katika kuwezesha mawasiliano ya utulivu kati ya Marekani na Iran.

Qatar imeendelea kuwa mwenyeji wa mazungumzo mbalimbali yanayohusisha Hamas na Taliban, huku Saudi Arabia ikiwa mstari wa mbele katika juhudi za kidiplomasia za kutafuta suluhu ya mgogoro wa Sudan.

Majukumu hayo yanaendana na maslahi mapana ya kijiopolitiki ya Marekani, na kwa sasa Pakistan imeingia katika mkondo huo. Inafanya kazi kama daraja la kupitisha ujumbe na kuratibu washirika mbalimbali wa kikanda. Hata hivyo, hii si mara ya kwanza kwa Pakistan kutekeleza wajibu wa aina hiyo.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah*



KALAMU HURU

SEHEMU YA 2

SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# Nini baada ya Hijja?

## Hijja ni shule ya uchamungu

Katika makala iliyopita tulijadili mafunzo ya Ihram na kuona jinsi ibada hiyo inavyomjenga Muislamu katika misingi ya uRehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yakea, unyenyekevu na nidhamu ya nafsi. Tuliona kuwa Hujaji huvua mavazi ya kawaida ili avae mavazi ya utiifu na kujikabidhi kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini swali kubwa linabaki: Je, mafunzo hayo yote yanaelekea katika lengo gani? Jibu lake ni moja: Taqwa (uchamungu).

Kwa hakika, Taqwa ndiyo roho ya Hijja na ndiyo tunda kuu ambalo Muislamu anatakiwa kulivuna kutoka katika ibada hii adhimu. Ikiwa Hijja imekamilika lakini haijamjengea mtu uchamungu, basi amepoteza sehemu kubwa ya hekima iliyokusudiwa ndani yake.

### Taqwa ni nini?

Wanazuoni wamefafanua kuwa Taqwa ni kujenga kinga baina yako na adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza amri Zake na kujiepusha na makatazo Yake.

Kwa lugha nyepesi zaidi, Taqwa ni kuishi maisha ya kumheshimu Mwenyezi Mungu kila mahali na katika kila hali.

Muislamu mwenye Taqwa si yule anayemkumbuka Mwenyezi Mungu msikitini pekee, bali ni yule anayemkumbuka pia akiwa sokoni, kazini, nyumbani na hata anapokuwa peke yake pasipo kuonekana na watu.

### Kwa nini Hijja inamjenga mtu kuwa na Taqwa?

Katika Qur'an, Mwenyezi Mungu anasema: "Na jipatieni masurufu; na hakika masurufu bora ni Taqwa." [Qur'an, 2:197]. Aya hii imekuja katika maelekezo ya Hijja, jambo linaloonesha kuwa safari ya Hijja si ya mwili pekee bali ni safari ya moyo.

Katika siku za Hijja, Muislamu hujifunza kuishi chini ya uangalizi wa Mwenyezi Mungu. Anaacha mambo fulani si kwa sababu yana madhara ya kidunia, bali kwa sababu ameamrishwa kuyaacha.

Hapa ndipo siri ya Taqwa ilipo.

Mtu anapojifunza kutii kwa sababu Mwenyezi Mungu ameamrisha, basi moyo wake huanza kuzoea kumtanguliza Mola wake Mlezi mbele ya matamanio ya nafsi.

### Arafa : Chuo kikuu cha Taqwa

Ikiwa Ihram ni darasa la kwanza la Taqwa, basi Arafa ni chuo chake kikuu.

Katika siku ya Arafa , mamilioni ya watu husimama chini ya anga moja, wakimuomba Mola mmoja, wakitarajia rehema moja.

Hakuna anayejivunia mali yake.

Hakuna anayejivunia cheo chake.

Hakuna anayejivunia nasaba yake.

Kila mmoja anakuja akiwa na haja moja kubwa: msamaha wa Mwenyezi Mungu.

Katika mazingira hayo, moyo wa Muislamu hujifunza ukweli muhimu kwamba mafanikio ya kweli hayapatikani kwa mali wala umaarufu, bali kwa ukaribu wake kwa Mwenyezi Mungu.

### Taqwa baada ya Hijja

Changamoto kubwa si kujenga Taqwa wakati wa Hijja bali kuendelea nayo baada ya kurejea nyumbani.

Ndani ya Makka mazingira yote humsaidia mtu kufanya ibada. Adhana husikika kila mahali, Qur'an husomwa kila kona na watu wengi wanaelekea katika utiifu.

Lakini baada ya kurejea katika maisha ya kawaida, mtu hukutana tena na biashara, kazi, marafiki, mitandao ya kijamii na vishawishi mbalimbali.

Hapo ndipo Taqwa inapopimwa.

Je, mtu ataendelea kulinda macho yake dhidi ya haramu?

Je, ataendelea kulinda ulimi wake dhidi ya uongo na fitina?

Je, ataendelea kutekeleza Swala kwa wakati wake?

Je, ataendelea kusoma Qur'an kama alivyokuwa akiisoma wakati wa Hija?

Maswali haya ndiyo yanayobainisha ikiwa Taqwa ya Hija imeendelea kuishi au imebakia kuwa kumbukumbu ya safari.

### Dalili za Taqwa ya kweli

Miongoni mwa alama za Taqwa baada ya Hijja ni kuongezeka kwa utii kwa Mwenyezi Mungu, kupungua kwa maasi na uzembe, kuwa mwangalifu katika haki za watu.

Alama nyingine ni kuongezeka kwa huruma na msamaha, kuhifadhi Swala na Qur'an na kujitahidi kufanya mema hata pale ambapo hakuna anayekuona.

Haya ndiyo matunda yanayotarajiwa kuonekana kwa mtu aliyefaidika na shule ya Hijja.

### Jamii inahitaji watu wa Taqwa

Leo Umma wa Kiislamu hauhitaji mahujaji wengi kwa idadi pekee. Unahitaji mahujaji wanaorudi na Taqwa.

Unahitaji viongozi wenye Taqwa.

Unahitaji wafanyabiashara wenye Taqwa.

Unahitaji wazazi wenye Taqwa.

Unahitaji vijana wenye Taqwa.

Kwa sababu Taqwa ndiyo msingi wa uadilifu, haki, amani na maendeleo ya jamii.

Mahali ambapo Taqwa ipo, haki huimarika. Na mahali ambapo Taqwa inapotea, hata sheria nyingi haziwezi kuzuia uovu.

### Hitimisho

Hijja ni shule ya Taqwa. Kila tendo ndani yake lina lengo la kumkaribisha mja kwa Mola wake Mlezi na kumjenga awe mwenye kumcha Mwenyezi Mungu katika siri na dhahiri.

Mafanikio ya Hijja hayapimwi kwa idadi ya safari zilizofanywa, bali kwa kiwango cha Taqwa kilichobaki moyoni baada ya safari kumalizika.

Lakini pamoja na kujenga Taqwa kwa mtu mmoja mmoja, Hijja pia hubeba ujumbe mkubwa kwa Umma mzima wa Kiislamu. Ni ujumbe ambao huonekana wazi pale mamilioni ya Waislamu kutoka kila pembe ya dunia wanapokusanyika katika sehemu moja, wakisema maneno yale yale na wakimwabudu Mola mmoja.

### Ni ujumbe wa umoja wa Umma wa Kiislamu.

Je, HiJja inatufundisha nini kuhusu umoja? Kwa nini pamoja na tofauti za lugha, rangi na tamaduni, Waislamu huonekana kama familia moja wakati wa Hijja? Na ni kwa namna gani

مُحرم

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 2 YA MWISHO

Na Said Rajab
0783 650 803

# Miaka 78 baada ya Nakba, nini kinafuata?



Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulijadili jinsi Mkataba wa Oslo, ambao ulikusudiwa kuleta amani ulivyowatia kitanzi Wapalestina. Zaidi ya miaka 32 tangu kusainiwa kwa makubaliano hayo, hakuna mabadiliko yoyote yaliyoonekana katika vitendo vya Mazayuni dhidi ya Wapalestina zaidi ya kuzidisha mauaji na kushambulia maeneo matakatifu ya Waislamu kule Jerusalam, Al–Khalil na kwingineko.

Pengine, swali la kujiuliza hapa ni hili. Kuna haja gani ya kudumisha makubaliano ambayo hayana chochote kilichobaki zaidi ya kuimarisha nguvu ya kundi teule ndani ya Mamlaka ya Palestina, na kuliruhusu kutumia rasilimali za wananchi wa Palestina kupitia kodi, tozo na ada mbalimbali?

Lengo ni kukomboa ardhi ya Wapalestina inayokaliwa kimabavu, au kutekeleza sera za Mazayuni, Marekani na Ulaya katika vita vyao dhidi ya Uislamu na Waislamu?

Ukombozi wa Yerusalemu usingechelewa kwa miaka 78 kama isingekuwa Mkataba wa Sykes–Picot, ambao ulisababisha kugawanywa kwa ardhi ya Waislamu na kuundwa kwa vidola vidogo vidogo vinavyodhibitiwa na mataifa ya Magharibi, baada ya kusambaratika kwa dola kubwa ya Kiislamu ya Uthmaniyyah (The Ottoman Empire) mwaka 1924.

Kila Muislamu ndani ya nchi hizo alifungwa na utii wa kitaifa. Matokeo yake, Waislamu hawakuendelea kuiona ardhi tukufu ya Palestina kama suala lenye uzito wa kipekee kwao, bali waliiona kama chanzo cha hisia za Kiislamu pekee. Wapo ambao hutokwa na machozi wanapoitaja, lakini hali hiyo hubaki katika kiwango cha hisia zaidi kuliko wajibu wa pamoja.

Kadri dhana za utaifa na uzalendo kwa nchi zilivyozidi kuimarika katika ulimwengu wa Waislamu, ndivyo makafiri walivyozidi kufanikiwa kuwachelewesha Waislamu kujipanga na kuelekea msikiti wa Al–Aqsa kwa ajili ya ukombozi wa Msikiti huu Mtukufu.

Kwa zaidi ya miaka 78, dola ya Kizayuni imeendeleza unyama wake kwa kasi ile ile, ikiongeza mauaji yake kwa Wapalestina, ikiwaletea njaa, unyang'anyi wa ardhi, na kugeuza matukufu ya Waislamu kuwa ya Kiyahudi.

Mkataba wa Sykes–Picot pamoja na watawala wa nchi za Kiarabu walifanikiwa kubadili mwelekeo wa suala la Palestina, kutoka katika lengo la kuing'oa dola hii haramu ya Kizayuni, hadi katika mjadala wa namna ya kuishi nayo kupitia makubaliano ya kurekebisha na kuimarisha uhusiano.

Kwa sisi Waislamu, msiba wetu mkubwa ulikuwa siku ile ambayo Waislamu walipoteza dola yao. Ardhi zetu zilipasuliwa vipande vipande, na kila adui wa karibu na wa mbali alianza kutunyemelea. Palestina ni sehemu moja tu ya mgogoro huu mkubwa.

Ufumbuzi wa suala la ardhi Tukufu ya Palestina upo katika kuirudisha kwenye njia yake ya kweli kama jambo la Waislamu wote duniani, na kuiweka mbali kabisa na upuuzi wa utaifa na taasisi za kimataifa, ambazo kwa miaka mingi sasa imethibitika kuwa ni udanganyifu na kupoteza muda.

محرم

# NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI



# Mafunzo ya Luqman yalivyobeba dira ya malezi

Malezi ya watoto ni miongoni mwa majukumu makubwa ambayo Mwenyezi Mungu amewakabidhi wazazi na walezi. Jamii yoyote inayotamani kuwa na mustakabali mwema lazima iwekeze katika malezi bora ya watoto, kwa kuwa watoto wa leo ndio viongozi, wasomi, wafanyabiashara na walezi wa kesho.

Ndiyo maana Uislamu umeweka misingi madhubuti ya malezi kupitia Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Miongoni mwa mifano bora ya malezi iliyohifadhiwa katika Qur'an ni nasaha za Luqman kwa mwanawe zilizotajwa katika Surat Luqman. Mafundisho haya yanabeba dira kamili ya malezi ya mtoto kwa kuwa yanagusa nyanja za imani, ibada, maadili, unyenyekevu na uwajibikaji.

Hadi leo, mawaidha ya Luqman yanaendelea kuwa mwongozo muhimu kwa wazazi na walezi katika kujenga kizazi chenye maadili mema na kinachomcha Mwenyezi Mungu. Luqmaan alimnasihi mwanawe kwa kumwambia: "Ewe mwanangu! Usimshirikishe Allah, hakika shirk ni dhuluma kubwa mno!" [Qur'an, 31:13].

Mafundisho haya yanaonesha kuwa msingi wa kwanza wa malezi ya mtoto ni kujenga imani sahihi. Luqman alianza kwa kumfundisha mwanawe Tauhidi, yaani kumuamini Mwenyezi Mungu Mmoja na kumuepusha na ushirikina.

Hii inaonesha kuwa kabla ya mtoto kufundishwa elimu za dunia, anapaswa kwanza kujengwa katika msingi wa kumjua Muumba wake na kutambua wajibu wake kwake.

Katika zama hizi ambazo watoto wanakabiliwa na ushawishi mkubwa kutoka katika mitandao ya kijamii, teknolojia na tamaduni mbalimbali, wazazi wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha watoto wao wanajengewa imani thabiti.

Mtoto anayemjua Mungu tangu utotoni huwa na uwezo mkubwa wa kutofautisha mema na mabaya, na huwa na hofu ya kufanya maovu hata pale asipoonekana na watu.

Baada ya kumfundisha Tauhidi, Luqman alimkumbusha mwanawe umuhimu wa kutambua ukuu wa Mwenyezi Mungu na kwamba hakuna jambo la siri mbele yake. Luqman alimwambia mwanawe: "Ewe mwanangu! Hakika jambo lolote lenye uzito wa punje ya hardali, likawa katika jabali au mbinguni au ardhini, Allah atalileta..." [Qur'an, 31:16].

Katika mazingira ya sasa, ambapo baadhi ya watoto hujihusisha na vitendo vya udanganyifu, wizi, matumizi mabaya ya teknolojia na tabia nyingine zisizofaa wakidhani hakuna anayewaona, mawaidha haya yanaweka msingi wa kujenga dhamira ya ndani inayomfanya mtoto kuwa mwadilifu hata akiwa peke yake.

Dira nyingine muhimu ya malezi inayopatikana katika mawaidha ya Luqman ni umuhimu wa sala. Luqman alisema: "Ewe mwanangu! Simamisha swala..." [Qur'an, 31:17].

Ibada ya sala ni msingi unaomjenga mtoto katika nidhamu, utiifu na ukaribu na Allah. Luqman alifahamu kuwa mtoto anayeshikamana na sala hukua akiwa na maadili bora na hofu ya Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, wazazi wanapaswa kuwa mfano bora kwa watoto wao katika utekelezaji wa ibada na kuwalea katika mazingira yatakayowafanya waipende dini yao.

Luqman hakusisitiza ibada pekee, bali pia alimhimiza mwanawe kuwajibika kwa jamii. Alisema: "Na amrisha mema na ukataze mabaya..." [Qur'an, 31:17]. Hii ni dira muhimu ya malezi inayowafundisha watoto kuwa sehemu ya suluhisho la matatizo yanayoikabili jamii.

Mtoto anapaswa kufundishwa kupenda haki, kusaidia wahitaji, kusimamia ukweli na kupinga maovu kwa hekima na busara. Jamii nyingi hivi sasa zinakabiliwa na changamoto ya mmomonyoko wa maadili kutokana na kukosekana kwa watu wanaothubutu kusimamia ukweli.

## Subira na unyenyekevu

Aidha, Luqman alimfundisha mwanawe umuhimu wa subira alipomwambia: "...na subiri katika yale yatakayokusibu..." [Qur'an, 31:17].

Katika dunia ya sasa yenye ushindani mkubwa, watoto hukutana na changamoto nyingi katika masomo, maisha ya kijamii na maendeleo yao binafsi. Wakikosa subira, wanaweza kukata tamaa, kupata msongo wa mawazo au hata kujihusisha na vitendo vinavyohatarisha maisha yao.

Kwa sababu hiyo, wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto kukabiliana na matatizo bila kukata tamaa. Mtoto anayejengwa katika misingi ya subira huwa na uwezo mkubwa wa kuvumilia changamoto na kufikia mafanikio katika maisha yake.

Jambo jingine linalovutia katika mawaidha ya Luqman ni jinsi alivyosisitiza unyenyekevu. Allah anasema: "Na wala usiwageuzie watu uso wako kwa kiburi, na wala usitembee katika ardhi kwa maringo..." [Qur'an, 31:18].

Aya hii inafundisha kuwa malezi bora hayapaswi kuishia katika elimu na ibada pekee, bali pia yanapaswa kujenga tabia njema. Kiburi ni miongoni mwa tabia mbaya zinazomfanya mtu awadharau wengine na kujiona bora kuliko wenzake.

Malezi ya Kiislamu humlea mtoto katika misingi ya maadili mema, heshima na kuwathamini wengine. Vilevile, humfundisha kutambua kwamba ubora wa mwanadamu haupimwi kwa mali, cheo au hadhi aliyonayo, bali kwa uchamungu na matendo mema.

## Adabu za mazungumzo

Luqman, pia alimfundisha mwanawe adabu za mazungumzo. Qur'an inasema: "Na ushushe sauti yako; hakika sauti mbaya zaidi ni sauti ya punda." [Qur'an, 31:19]. Kupitia mawaidha haya, tunajifunza kuwa malezi ya Kiislamu yanazingatia hata namna ya kuzungumza.


Mtoto anapaswa kufundishwa heshima, ustaarabu na busara katika mawasiliano yake na wengine. Lugha nzuri ni alama ya malezi bora na huchangia kujenga uhusiano mzuri katika familia na jamii kwa ujumla.

Katika kipindi hiki ambacho matumizi ya mitandao ya kijamii yameongezeka, watoto

DARASA LA WIKI

SHEIKH Seif Ruga
0712 690 811

# Fanya haya kuepuka tatizo la afya ya akili



Katika dunia ya sasa yenye pilikapilika nyingi, afya ya akili imekuwa nguzo muhimu katika maisha ya mwanadamu na hitaji la msingi kwa uwiano na utulivu wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

Ingawa nadharia na vyuo mbalimbali vinavyotoa elimu ya saikolojia vimeonesha umuhimu mkubwa wa afya ya akili, mwenye kutafakari mwongozo wa Uislamu atagundua kuwa dini hii imewasilisha mtazamo kamili na wa kina kuhusu afya ya akili.

Mtazamo huu hauishii kwenye nadharia pekee, bali unaingia moja kwa moja katika maisha ya kila siku, ukiunganisha kwa ustadi mkubwa chakula cha kiroho, malezi ya tabia na maadili mema pamoja na msaada wa kijamii katika mfumo unaolenga kufanikisha "nafsi iliyotulia", ambayo Allah ameitaja katika Qur'an Tukufu: "Ewe nafsi iliyotulia! Rejea kwa Mola wako hali ya kuwa umeridhika na umeridhiwa." [Qur'an, 89:27–28].

Kwa hiyo, ni muhimu kufafanua misingi ya mtazamo huu wa Kiislamu kuhusu afya ya akili na kuonesha jinsi Uislamu ulivyoweka kanuni imara za kuleta uwiano kati ya mwili, roho na akili.

Vilevile, ni lazima kusisitiza umuhimu wa kutumia sababu halali na kutafuta msaada wa wataalamu pale inapohitajika, kwani kufanya hivyo hakupingani na kumtegemea Allah Mtukufu, bali ni sehemu ya kutekeleza maelekezo ya sharia tukufu ya Kiislamu.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, nafsi si mkusanyiko wa fikra au hisia za muda mfupi pekee, bali ni kiini cha utu wa mwanadamu, kituo cha utambuzi, hisia na maamuzi. Ni mfumo unaojumuisha roho, mwili na akili, huku ukivutwa na nguvu za kheri na za shari.

Qur'an Tukufu imetaja aina mbalimbali za nafsi, miongoni mwazo ni nafsi yenye kuamrisha maovu, ambayo huelemea matamanio na upotovu. Pia kuna nafsi yenye kujilaumu ambayo humkosoa mtu kwa makosa yake na kumhimiza kujirekebisha na kufikia ukamilifu.

Vilevile kuna nafsi iliyotulia ambayo hupata utulivu wa moyo na amani ya ndani kupitia utiifu kwa Allah na kujikurubisha kwake.

Lengo la malezi ya Kiislamu ni kuinua nafsi kutoka katika hali ya kughafilika na kufuata matamanio, na kuipeleka katika hali ya uchamungu, mwamko wa kiroho na utulivu wa moyo. Hali hii ndiyo msingi wa afya ya akili ya kweli, huku Uislamu ukiipa nafasi kubwa upande wa kiroho kama msingi wa afya ya akili.

## Nguzo sita za kukabili tatizo la afya ya akili

Miongoni mwa nguzo muhimu za kukabiliana na tatizo la afya ya akili ni kumdhukuru Allah kwa namna mbalimbali, ikiwa ni pamoja na tasbihi, tahmidi, takbiri na tahlili, pamoja na kusoma Qur'an, ambayo ni dawa ya nyoyo za waumini na ufunguo wa utulivu wa nafsi.

Allah anasema: "...Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu nyoyo hutulia." [Qur'an, 13:28].

### Pili, kusimamisha sala

Sala ni nguzo ya dini na kiungo kinachohuisha kila siku uhusiano kati ya mja na Mola wake. Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akimwamuru Bilal (Allah amridhie) alete wito wa kuanza sala, akisema: "Ewe Bilal, tupumzishe (tupe raha ya moyo) kwa swala." [Abu Daudi].

Kadhalika, dua ni silaha ya muumini. Kupitia dua, mtu humueleza Allah udhaifu wake, mahitaji yake na matumaini yake, hali inayopunguza mzigo wa matatizo katika nafsi na kuleta matumaini mema.

### Tatu, subira na kumtegemea Allah

Imani kwamba kila jambo linalotokea limo katika elimu, hekima na makadirio ya Allah Mtukufu huipa nafsi hisia ya usalama, subira na utulivu.

Subira ndiyo ufunguo wa faraja na ni tabia adhimu inayomfundisha mwanadamu kuvumilia, kusimama imara na kutokata tamaa anapokumbana na matatizo. Allah anasema: "Wape bishara njema wenye kusubiri." [Qur'an, 2:155].

### Nne, kukumbuka neema za Allah

Kukumbuka neema za Allah Mtukufu na kumshukuru huujaza moyo ridhaa na furaha. Allah Mtukufu anasema: "Mkishukuru, bila shaka nitakuzidishieni." [Qur'an, 14:7]. Aidha, Uislamu unahimiza kuwa na matumaini na unakataza kukata tamaa pamoja na kuwa na fikra za shari kuhusu mambo yajayo.

Tano, kushikamana na tabia njema

Kujipamba na tabia njema kama kusamehe, kuvumilia makosa ya wengine na kuwahurumia wenye mahitaji husafisha moyo dhidi ya chuki.

Uislamu unasisitiza umuhimu wa kuishi kwa maadili mema ya dini, ambayo huchukuliwa kuwa kinga ya nafsi dhidi ya misukosuko na hisia hasi zinazoweza kuathiri afya ya akili.

### Sita, kuamiliana vizuri na watu

Uislamu haukupuuza umuhimu wa mazingira mazuri ya kijamii katika kuimarisha afya

NA ZAHARANI BARAKA

مُحرم

MATUKIO
YENYE MAZINGATIO

# Mbinu rahisi za kumshinda shetani

**Kutoka kwa Abu Dardaa (Allah amridhie) amesema kuwa, siku moja Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) alisimama kusali, wakamsikia akisema: "Najikinga kwa Allah dhidi yako."**
**Kisha akasema mara tatu: "Nakulaani kwa laana kamili ya Allah," huku akinyoosha mkono wake kana kwamba anataka kushika kitu.**
**Alipomaliza sala, tukasema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Tumekusikia ukisema ndani ya sala maneno ambayo hatukuwahi kukusikia ukiyasema hapo kabla, na pia tumekuona ukinyoosha mkono wako."**
**Mtume akasema: "Hakika adui wa Allah, Iblisi, alikuja akiwa na mwenje wa moto ili aueleekeze usoni mwangu. Nikasema mara tatu: 'Najikinga kwa Allah dhidi yako.' Kisha nikasema mara tatu: 'Nakulaani kwa laana kamili ya Allah,' lakini hakurudi nyuma. Nikataka kumkamata.**
**Naapa kwa Allah! Kama si dua ya ndugu yetu Suleiman (amani imshukie), Iblisi angekuwa amefungwa, na watoto wa Madina wangekuwa wakicheza naye." *[Muslim]*"**

## Mafundisho ya hadith

Mtume (rehema na amani zimshukie) ametaja dua ya Nabii Suleiman (amani imshukie) aliposema: "Mola wangu! Nisamehe na unipe ufalme ambao hutampa yeyote baada yangu."

Dua hii ndiyo iliyomzuia Mtume kumkamata Iblisi na kumfunga, kisha kuwaacha watoto wa Madina wakimchezea. Kwa sababu ya dua hiyo, Mtume (rehema na amani zimshukie) hakumkamata Iblisi ili mamlaka hayo maalumu yabaki kuwa miongoni mwa mambo aliyotunukiwa Nabii Suleiman (amani imshukie) pekee.

## Uadui wa Iblisi kwa waja wema

Iblisi alikwenda kumfanyia uadui Mtume (rehema na amani zimshukie) alipokuwa akisali. Ikiwa Mtume hakusalimika na majaribio ya Iblisi, basi watu wengine wako katika hatari zaidi.

Allah anasema: "Hakika shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa adui..." [Qur'an, 35:6]. Pia amesema: "Hakika shetani anataka kutia uadui na chuki baina yenu." [Qur'an, 5:91]. Watu wema ndiyo wanaolengwa zaidi na Iblisi kwa sababu wanamtii Allah na wanawaongoza wengine katika kheri.

## Umuhimu wa kujikinga na Iblisi

Mtume (rehema na amani zimshukie) alipokabiliwa na Iblisi hakutegemea nguvu zake, bali alimwelekea Allah na kusema: "Najikinga kwa Allah dhidi yako."

Hii inaonesha kuwa kinga bora dhidi ya shetani ni kumkimbilia Allah Ta'ala, kama alivyosema: "Na kama ukichokozwa na shetani kwa uchokozi wowote, basi jikinge kwa Allah..." [Qur'an, 7:200].

Miongoni mwa njia za kujikinga na shetani ni kusoma adhkari za asubuhi na jioni, Ayatul Kursiy, Suratul Falaq, Suratun Naas, pamoja na kudumisha sala na dhikri.

Moja ya sababu zinazofanya vita dhidi ya shetani kuwa ngumu ni kwamba yeye anatuona ilhali sisi hatumuoni. Allah anasema: "Hakika yeye na kundi lake wanawaona kutoka mahali ambapo nyinyi hamuwaoni." [Qur'an, 7:27].

Kwa sababu hiyo, Muislamu anatakiwa kuwa macho wakati wote na asidharau maasi madogo wala wasiwasi wa shetani, bali ajikurubishe kwa Allah, Mjuzi wa mambo ya siri na ya dhahiri.

Watu wengi wameangukia kwenye mitego ya shetani kwa sababu ya kufuata matamanio ya nafsi na kuacha mwongozo wa Allah. Qur'an inasema: "Na kwa yakini (shetani) amepoteza wengi mno miongoni mwenu." [Qur'an, 36:62]. "Na watu wengi hawataamini hata ukitamani vipi." [Qur'an, 12:103].

Aya hizi zinatukumbusha kutotegemea wingi wa watu, bali kuifuata haki hata kama wanaoifuata ni wachache.

## Iblisi atawakana wafuasi wake Siku ya Kiyama

Baada ya kuwapotosha watu duniani, Iblisi atajitenga nao na kuwakana mbele ya Allah. "Na shetani atasema itakapopitishwa hukumu: Hakika Allah alikuahidini ahadi ya haki (na ameitimiza), nami nilikuahidini kisha nikakukhalifuni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu isipokuwa nilikuiteni mkaniitikia. Basi msinilaumu, bali zilaumuni nafsi zenu. Mimi siwezi kukuokoeni wala nyinyi hamuwezi kuniokoa..." [Qur'an, 14:22].

Katika aya nyingine, Allah Ta'ala anasema: "Ni kama shetani alipomwambia mtu: 'Kufuru,' na alipokufuru akasema: 'Hakika mimi najitenga nawe! Mimi namhofu Allah, Mola wa walimwengu.'" [Qur'an, 59:16].

Hivi ndivyo shetani atakavyokana uhusiano wake na wafuasi wake, akidai kwamba kazi yake ilikuwa ni ushawishi tu. Hakumlazimisha mtu kumtii wala hakuwa na uwezo wa kumteza nguvu.

## Udhaifu wa Iblisi kwa wachamungu

Imepokewa hadith kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) kwamba Mtume (rehema na amani zimshukie) alimtuma kusimamia na kuhifadhi Zakatul–Fitri. Wakati wa utekelezaji wa jukumu hilo, alitokea mtu mmoja ambaye alianza kuchota chakula cha zaka kwa mikono yake. Tukio hilo lilijirudia kwa siku tatu mfululizo.

Alipojaribu kuchota chakula hicho kwa mara ya tatu, Abu Huraira alimkamata na kumwambia: "Nitakupeleka kwa Mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie)." Hata hivyo, mtu yule alimwomba amwachie huku akisema: "Nikufundishe maneno ambayo Allah atakufaidisha kwayo." Abu Huraira akamuuliza: "Ni maneno gani hayo?"

Akajibu: "Utakapoingia kitandani kulala, soma Ayatul Kursiy. Ukifanya hivyo, Allah ataendelea kukulinda, na shetani hatakukaribia hadi asubuhi." Asubuhi ilipowadia, Mtume (rehema na amani zimshukie) akamuuliza Abu Huraira kuhusu yaliyotokea usiku huo.

Baada ya kumsimulia kila kitu, Mtume akasema: "Amekwambia kweli, japokuwa ni mwongo." Kisha akamuuliza: "Je, unajua ni nani ambaye ulikuwa ukizungumza naye katika siku hizo tatu?" Mtume akaeleza: "Huyo alikuwa shetani." [Bukhari].

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 12

مُحرم



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## Rajulun mu'min ajitokeza kumtetea Musa

Baada ya Fir-aun kushindwa vibaya kwenye mapambano na kupelekea hatimaye wachawi kusilimu, Fir-aun alitangaza kumuua Musa.

Tangazo hilo lilimtoa mtu mmoja ambaye Qur'an haikutaja jina lake bali ilimuelezea kama 'Rajulun muumin' (yaani mtu aliyemuamini Allah na kumfuata Musa akaficha Imani yake) na kumtetea Musa.

Qur'an inasema: "Na akasema mtu mmoja Muislamu aliyekuwa mmoja wa watu wa Fir-aun afichaye Imani yake, 'Oh! Mwataka kumuua mtu kwa sababu anasema Mola wangu ni Mwenyezi Mungu na kwa hakika amekujieni kwa dalili za wazi zitokazo kwa Mola wenu! (msimuuwe) akiwa ni muongo basi uongo wake utamdhuru mwenyewe, na akiwa ni mkweli yatakufikeni (duniani) baadhi ya anayokuahidi, bila shaka Mwenyezi Mungu hamuongozi apindukiaye mipaka muongo.'"

Jina la muumini huyo inasemekana ni mtoto wa ami wa Fir-aun. Akaendelea kuwanasihi watu wake kwa kusema: "Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika nchi; basi ni nani atakayenisaidia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia? Firauni akasema, 'Sikupeni shauri ila ile niliyo ona, wala sikuongozeni ila kwenye njia ya uwongofu."

Na yule aliyeamini akasema: 'Enyi watu wangu, hakika mimi nakuhofieni mfano wa siku za (adhabu iliyoyafika) makundi (ya maadui wa Mwenyezi Mungu) mfano wa hali ya watu wa Nuhu, na Adi, na Thamoud na wale waliokuja baada yao, na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu waja wake." [Qur'an, 40:28-31].

Muumini huyo aliendelea kuwaasa watu wake akasema: "Na enyi jama zangu, mimi nakuhofieni siku ya kuitana (kupiga makelele ya adhabu) siku mtakapogeuka kurudi nyuma (mutake kukimbia, na hamna pa kukimbilia), hamtakuwa na mlinzi kwa Allah na mwenye kuhukumiwa na Allah kupotea basi huyo hana muongozi yoyote" [Qur'an, 40:32-33].

Muumini huyo aliwakumbusha jamaa zake (wazee wao) upinzani wao kwa Mtume Yusuf akasema: "Na bila shaka zamani (huko) alikujieni Yusuf kwa dalili zilizo wazi lakini nyinyi mliendelea kuwa katika shaka kwa yale aliyokuleteeni, mpaka alipofariki mkasema, 'Mwenyezi Mungu hataleta Mtume baada yake'. kama hivi Mwenyezi Mungu humuacha kupotea yule anayepindukia mipaka katika maasi anayejitia shaka." [Qur'an, 40:34].

" Na yule aliyeamini aliendelea kusema: enyi watu wangu nifuateni nitakuongozeni njia ya uongofu. Enyi watu wangu, kwa hakika maisha ya dunia hii ni starehe (ipitayo tu) na bila shaka akhera ndiyo nyumba ya kukaa daima." [Qur'an, 40:38-39].

"Na enyi watu wangu, kwa nini mimi nakuiteni katika uokofu na nyinyi mnaniita kwenye moto!? Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na kumshirikisha na yule ambaye simjui nami nakuiteni kwa Mwenye nguvu, Mwingi wa msamaha. Bila shaka (kwa dhati kabisa) mnaniita kwenye kuwaabudu ambao hawana wito katika dunia wala akhera, na marejeo yetu ni kwa Allah, na wanaopindukia mipaka hao ndio watu wa motoni

"Karibuni hivi mtayakumbuka ninayokuambieni (mawaidha yangu), nami ninamkabidhi mambo yangu Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anawaona waja wake." [Qur'an, 40:41-44].

### Mazingatio:

Katika nasaha zake "Rajulun mu'min" kwanza alimtetea Musa, na hakuona sababu ya msingi ya kuhukumiwa kifo. Kama masala ya kuwaita watu kwenye Imani (dini) yake, basi kila mtu ana uhuru wa kufuata na kuitangaza dini yake.

Kwa maana nyengine, jamaa huyo alisisitiza kuheshimu uhuru wa kuabudu, kwa vile Musa amekuja na hoja zilizo wazi wala hazungumzi kiupia-upia (kibubusa).

Pili, nasaha zake hapo tena zikajikita katika kadhia ya akida (Imani) hususan juu ya akhera. Alibainisha kuwa, mja atafanikiwa kwa kupata msamaha, radhi na pepo ya Allah iwapo ataamini na kufanya matendo mema. Lakini aliyekufuru na kupuuza maagizo ya Allah, makazi yake huko akhera ni motoni.

Aliwatahadharisha na adhabu mbaya kwa kuwakumbusha yaliyowafika watu waliopita: akina Adi, Thamoud na watu wa Mtume Nuhu (amani ya Allah iwashukie).

Kwa ujumla, nasaha za mja huyo zilikuwa na mantiki na faida kubwa kwa Fir-aun na watu wake kama wangelizisikiliza na kuzifanyia kazi. Lakini wapi! walimpinga na wakataka kumuua, Mwenyezi Mungu akamuokoa.

Qur'an inasema: "Allah akamuokoa na ubaya wa hila walizozipanga, na adhabu mbaya ikawazunguka watu wa Fir-aun (pamoja na mwenyewe) [Qur'an, 40:45].

### Watu wa Musa wamlalamikia

"Wakasema, 'Tumeudhiwa kabla hujatujia na (sasa) baada ya wewe kutujia. (Musa) akasema, 'Asaa Mola wenu atamuangamiza adui yenu na kukufanyeni watawala katika nchi (hii) na aone jisi mtakavyofanya." [Qur'an, 12:129].

*Itaendelea inshaAllah*

# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

UONGOZI
UTAWALA

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# Jinsi ya kufanya kazi na bosi mpenda sifa bila kupoteza weledi



Katika maisha ya kazi, si kila changamoto hutokana na ugumu wa majukumu au uhaba wa rasilimali. Wakati mwingine changamoto kubwa huwa mtu unayemripoti kwake kila siku.

Wafanyakazi wengi wamewahi kufanya kazi chini ya bosi anayependa kutambuliwa kila wakati, anayependa mawazo yake yashinde, na ambaye hapokei kwa urahisi maoni yanayopingana na yake.

Watu wengi wanapokutana na bosi wa aina hii huingia katika moja ya mitego miwili. Wapo wanaochagua kupambana naye katika kila jambo, hali inayozalisha migogoro isiyoisha. Wengine huamua kujisalimisha kabisa, wakikubali kila kitu hata pale wanapoona wazi kuwa kuna tatizo. Njia zote mbili huwa na gharama zake.

Kwa kweli, siri ya kufanya kazi na bosi mwenye mpenda sifa si kupambana naye wala kujipendekeza kwake. Ni kujifunza namna ya kusimamia mahusiano hayo kwa akili, busara na ustadi wa mawasiliano.

## Mfahamu kwanza unayeshughulika naye

Hatua ya kwanza ni kutambua kwamba si kila mtu mwenye kujiamini ana tatizo la kupenda sifa. Wengine ni viongozi wenye maono makubwa, wanaojua wanachokitaka na wanaojiamini katika maamuzi yao. Lakini kuna tofauti kati ya kujiamini na kutawaliwa na kupenda sifa.

Bosi mpenda sifa mara nyingi hupenda kuthibitishwa. Anaweza kuchukua maoni tofauti kama mashambulizi binafsi. Anaweza kutaka mafanikio yaonekane yametokana na uongozi wake, na wakati mwingine akawa mgumu kukubali makosa.

Kadri unavyoelewa tabia yake, ndivyo unavyoweza kupanga namna ya kuwasiliana naye kwa ufanisi. Watu wengi hushindwa si kwa sababu wana hoja mbaya, bali kwa sababu wanawasilisha hoja nzuri kwa njia ambayo bosi wao haiwezi kuipokea.

## Mpe heshima anayohitaji, lakini usijishushe

Watu wengi huchanganya diplomasia na kujipendekeza. Ukweli ni kwamba kuna tofauti kubwa kati ya kumheshimu mtu na kujishusha mbele yake.

Bosi mpenda sifa mara nyingi hupenda kuhisi kuwa mamlaka yake yanatambuliwa. Hivyo unapowasilisha wazo jipya, usianze kwa kubomoa mawazo yake. Anza kwa kutambua mchango wake au mwelekeo aliouweka, kisha ongeza pendekezo lako.

Mfano, badala ya kusema, "Mpango huu hautafanya kazi," unaweza kusema, "Nadhani msingi wa wazo hili ni mzuri, na tunaweza kupata matokeo bora zaidi tukiongeza kipengele hiki." Lengo si kumdanganya. Lengo ni kupunguza upinzani usio wa lazima ili hoja yako isikilizwe.

## Jifunze kutoa sifa na kuwashirikisha katika maamuzi

Katika mazingira ya kazi, kutoa sifa kwa viongozi wako pale inapostahili ni mbinu ya busara. Bosi anapohisi kuwa mafanikio ya timu yanamfanya naye aonekane vizuri, huwa na uwezekano mkubwa wa kukuamini na kukuunga mkono.

Vilevile, watu wengi hupinga mawazo si kwa sababu ni mabaya, bali kwa sababu hawakushirikishwa katika kuyaunda. Ndiyo maana wakati mwingine ni bora kuwasilisha chaguzi mbili au tatu badala ya hitimisho moja la mwisho.

## Ukitaka kupinga, tumia takwimu badala ya hisia

Mojawapo ya makosa makubwa wafanyakazi hufanya ni kuingia kwenye mabishano ya moja kwa moja na bosi mpenda sifa. Kadri mjadala unavyokuwa wa kihisia, ndivyo uwezekano wa kufikia suluhisho unavyopungua.

Badala yake, tumia ushahidi, takwimu na matokeo. Usiseme, "Nadhani una makosa." Sema, "Takwimu hizi zinaonesha kuwa njia hii inaweza kuleta matokeo bora zaidi."

Pia elekeza hoja zako kwenye maslahi yake. Watu wapenda sifa nyingi hujiuliza, "Hili lina maana gani kwangu?" Ukionyesha jinsi pendekezo lako litakavyosaidia mafanikio yake, timu yake au taswira yake, utakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kushawishi.

Epuka umbea na jifanye mshirika wa kimkakati

Bosi mpenda sifa mara nyingi huwa makini sana kuhusu kile watu wanachosema kumhusu. Ndiyo maana kujiingiza kwenye umbea wa ofisini ni hatari.


Badala ya kujijenga kama mkosoaji wake mkuu, jenga taswira ya mtu anayesaidia kutatua matatizo. Watu wa aina hii wanawathamini wale wanaowaona kama washirika wa mafanikio yao. Hii haimaanishi kukubaliana nao kila wakati. Inamaanisha kuwa hata unapopinga, unapinga kama mtu anayetafuta suluhisho, si kama mtu anayetafuta ushindi wa binafsi.

مُحرم

## TUJIFUNZE

### AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama



# Afrika iko wapi katika mbio za vumbuzi za AI?

Katika wiki za karibuni, habari mbili kutoka pande tofauti za dunia zilibeba ujumbe mmoja muhimu kuhusu mustakabali wa uchumi na elimu duniani.

Habari ya kwanza ilitoka China. Kati ya mwaka 2021 na 2025, vyuo vikuu nchini humo vilifuta au kusitisha zaidi ya programu 12,000 za shahada na kuanzisha zaidi ya programu mpya 10,000 zinazolenga akili mnemba (AI), sayansi ya data, roboti na teknolojia za hali ya juu. Lengo ni kuandaa wahitimu wanaohitajika katika uchumi wa kesho.

Habari ya pili ilitoka Marekani. Watafiti wa Kliniki ya Mayo walitangaza kuwa mfumo wa AI umefanikiwa kugundua dalili za saratani ya kongosho hadi miaka mitatu kabla ugonjwa haujaonekana kwa njia za kawaida za uchunguzi. Ugonjwa ambao kwa muda mrefu umekuwa miongoni mwa hatari zaidi sasa unaanza kukabiliwa kwa msaada wa teknolojia.

Kwa mtazamo wa haraka, habari hizi zinaonekana tofauti. Moja inahusu elimu, nyingine afya. Lakini zote zinaonesha jambo moja: dunia tayari ipo katikati ya mapinduzi ya akili mnemba.

## Swali ni hili: Afrika ipo wapi?

China inaandika upya mitaala yake. Marekani inawekeza mabilioni ya dola katika AI kwa ajili ya tiba, viwanda, elimu na utafiti. Mataifa mengine yanafanya vivyo hivyo. Yanajiuliza ni ujuzi gani utahitajika miaka 10 au 20 ijayo, kisha yanabadilisha mifumo yao ya elimu ili kujiandaa.

## Afrika bado inaonekana kusuasua.

Katika nchi nyingi, vyuo vikuu vinaendelea kuzalisha wahitimu kwa kutumia mitaala iliyoundwa kwa mahitaji ya uchumi wa zamani. Kila mwaka maelfu ya vijana wanahitimu wakiwa na vyeti, lakini mara nyingi bila ujuzi unaohitajika katika soko jipya la ajira linaloendeshwa na teknolojia, data na ubunifu.

Somo kutoka China si kwamba masomo ya sanaa, lugha au sayansi za jamii hayana umuhimu. Hata wachambuzi wa elimu nchini humo wameeleza kuwa mageuzi hayo yanalenga zaidi kuondoa programu zisizoendana na mahitaji ya sasa na kuimarisha zile zenye mchango mkubwa kwa jamii na uchumi.

Swali la msingi kwa Afrika si taaluma zipi zifutwe, bali kama tunafundisha kile kitakachohitajika kesho.

## AI inaweza kusaidia kila fani

Je, wanafunzi wa sheria wanafundishwa kuhusu AI katika mfumo wa sheria? Je, wanafunzi wa uandishi wa habari wanafundishwa matumizi ya AI katika uchambuzi wa taarifa? Je, wanafunzi wa tiba wanaandaliwa kwa zama ambazo mashine zitasaidia kugundua magonjwa mapema kuliko binadamu?

Tukikosa kujibu maswali haya, tutakuwa tunawaandaa vijana wa jana kwa ajili ya dunia ya kesho.

Wakati huo huo, maendeleo katika sekta ya afya yanaonesha ukubwa wa mabadiliko yanayokuja. AI inayoweza kuona dalili za saratani miaka kadhaa kabla ya ugonjwa kujitokeza si ndoto tena. Ni teknolojia inayojaribiwa sasa.

Kwa Afrika, hili linapaswa kuwa fursa. Bara lenye upungufu wa madaktari, walimu na wataalamu linaweza kutumia AI kuongeza tija na kupanua huduma muhimu. Lakini hilo haliwezi kutokea kwa kutegemea teknolojia zinazotengenezwa na wengine pekee.

Historia inaonesha kuwa mataifa yanayonufaika zaidi na mapinduzi ya kiteknolojia si yale yanayonunua teknolojia, bali yale yanayoitengeneza.

Ndiyo maana swali muhimu leo si kama AI itafika Afrika. Tayari imefika.

Swali ni kama Afrika itakuwa mtumiaji wa akili mnemba au mmoja wa watengenezaji wake. Kwa sababu wakati wengine wanabadilisha vyuo vikuu vyao na kutumia AI kuokoa maisha ya watu, sisi hatupaswi kuwa tunajiuliza kama mabadiliko yanakuja.

Tunapaswa kujiuliza kama tuko tayari kuyakabili.

مُحرم

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Kutembea: mazoezi rahisi yenye faida kubwa kwa afya

Watu wengi wanapotaka kuanza kufanya mazoezi, jambo la kwanza linalokuja akilini ni kujiunga na gym, kununua vifaa vya mazoezi au kuanza programu ngumu za mafunzo. Hata hivyo, wataalamu wa afya wanakubaliana kwamba mojawapo ya mazoezi rahisi, salama na yenye manufaa makubwa ni kutembea.

Kutembea hakuhitaji vifaa vya gharama kubwa, ujuzi maalumu wala mazingira ya kipeke bali muda, viatu vinavyofaa na dhamira ya kuanza. Licha ya urahisi wake, kutembea kunaweza kusaidia kupunguza mafuta mwilini, kuboresha afya ya moyo, kuimarisha mifupa, kusaidia mzunguko wa damu, kuboresha usingizi na hata kuongeza utulivu wa kihisia.

## Anza na malengo yanayowezekana

Moja ya sababu zinazowafanya watu wengi kuacha mazoezi mapema ni kuanza kwa matarajio makubwa kupita kiasi. Mtu ambaye hajafanya mazoezi kwa muda mrefu anaweza kuamua kutembea dakika 45 kila siku kuanzia siku ya kwanza. Baada ya siku chache anajisikia kuchoka, anaumwa misuli na hatimaye anaacha kabisa.

Njia bora ni kuanza kidogo na kujenga taratibu. Ikiwa dakika 20 zinaonekana nyingi, anza na dakika 10 mara tatu au nne kwa wiki. Kadiri mwili unavyozoea, ongeza dakika chache kila wiki. Baada ya kufikia lengo lako la muda, unaweza kuongeza kasi ya kutembea au kuchagua njia zenye miteremko zaidi ili kuongeza changamoto.

## Weka kutembea kwenye ratiba yako

Watu wengi husubiri mpaka wapate muda wa kutembea. Tatizo ni kwamba muda huo mara nyingi hauji.

Ndiyo maana ni muhimu kulifanya zoezi hili kuwa sehemu ya ratiba yako rasmi. Ikiwa unapenda kuamka mapema, tenga muda wa kutembea kabla ya shughuli nyingine kuanza. Ikiwa jioni ndiyo muda unaokufaa zaidi, weka muda huo kwenye ratiba yako kama unavyoweka miadi nyingine muhimu.

Unapotenga muda maalumu, kutembea huacha kuwa jambo la kufanya ukiwa huna kazi na kuwa sehemu ya maisha yako ya kawaida.

## Tembea na wengine

Kutembea peke yako kunaweza kuwa vizuri, lakini kutembea na mwingine kuna faida zake.

Mbali na kupata mazoezi, unapata nafasi ya kuzungumza, kubadilishana mawazo na kuimarisha mahusiano. Aidha, unapokuwa na mtu anayekusubiri, uwezekano wa kughairi unapungua.

Baadhi ya watu huanzisha utaratibu wa kutembea na marafiki zao kila siku au kila wiki. Wengine hutumia muda huo kuzungumza na wenzi wao wa ndoa au watoto wao. Hivyo, kutembea kunakuwa si tu zoezi la mwili, bali pia zoezi la kuimarisha mahusiano.

## Chagua vifaa vinavyofaa

Ingawa kutembea hakuhitaji vifaa vingi, viatu ni jambo muhimu sana.

Viatu vizuri vya kutembea vinapaswa kuwa na ulaini wa kutosha, kuruhusu hewa kupita na kukaa vizuri mguuni. Vidole vya miguu vinapaswa kuwa na nafasi ya kutosha kusogea bila kubanwa. Ikiwa viatu vinasababisha maumivu, malengelenge au michubuko, kuna uwezekano havikufai.

Mavazi pia yanapaswa kuwa mepesi, yenye kuruhusu hewa kupita na yanayokuwezesha kusogea kwa uhuru. Ikiwa hali ya hewa ni ya baridi, kuvaa nguo za tabaka kadhaa kunaweza kusaidia ili uweze kupunguza baadhi yake mwili unapopata joto.

## Fanya kutembea kuwa sehemu ya maisha ya kila siku

Si lazima kila kutembea kuwe mazoezi rasmi.

Wakati mwingine unaweza kuongeza hatua zako za kila siku kwa kufanya maamuzi madogo. Badala ya kutumia gari kwa safari fupi, unaweza kutembea. Badala ya kuegesha gari karibu kabisa na jengo, unaweza kuegesha mbali kidogo. Unaweza pia kutembea kwenda kituoni, dukani au kwenye shughuli nyingine za karibu.

Ukianza kuangalia kwa makini ratiba yako ya kila siku, utagundua fursa nyingi za kuongeza hatua bila kubadilisha sana maisha yako.

## Kuwa na mpango mbadala

Kutakuwa na siku za mvua, siku za uchovu na siku ambazo ratiba itakuwa imebanwa.

Hiyo haipaswi kuwa sababu ya kuacha kabisa. Ikiwa huwezi kutembea nje kwa sababu ya hali ya hewa, tafuta eneo la ndani kama jengo kubwa, ukumbi au sehemu nyingine salama. Ikiwa umekosa muda asubuhi, jaribu kutembea wakati wa mapumziko ya mchana au jioni.

## Kilicho muhimu si ukamilifu, bali mwendelezo.

Fuatilia maendeleo yako na kunywa maji ya kutosha




MAKALA MAAKUM

NA ZAHARANI BARAKA

# Mabadiliko yanayohitajika baada ya kuhiji

**Ibada ya Hijja imefaradhishwa kwa malengo mahsusi ya kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya Muislamu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhusiano mwema wa kijamii kwa mujibu wa mafundisho ya dini.**
**Athari za Hijja zinapaswa kuonekana kwa hujaji tangu anaporejea kutoka Hijja, na kuendelea kujidhihirisha katika nyanja zote za maisha kupitia uhusiano wake na watu na mwenendo wake wa kila siku.**
**Ni muhimu kutafakari mafunzo yatokanayo na Hijja ili mahujaji wafikie malengo yaliyokusudiwa na ibada hii.**

## Manufaa makubwa ya Hijja

Mahujaji wanapaswa kutambua kuwa wamepata manufaa makubwa kupitia ibada ya Hijja, ikiwamo kusamehewa madhambi yao na kurejea katika usafi wa kiroho kama walivyokuwa siku walipozaliwa.

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kuhiji, kisha asiseme maneno machafu wala kutenda maasi, atarejea akiwa msafi wa dhambi kama siku aliyozaliwa na mama yake." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaonesha ubora wa Hijja iliyokubaliwa, ambayo hufuta madhambi ya mja. Hivyo, baada ya kupata neema hiyo kubwa, hujaji anapaswa kutoyarejea maasi na kuendelea kuhifadhi usafi wa daftari lake la matendo.

## Malezi ya uchamungu

Mwenyezi Mungu anasema: "Na chukueni akiba; na hakika bora ya akiba ni uchamungu." [Qur'an, 2:197]. Aya hii imekuja katika muktadha wa mafunzo ya Hijja na imehitimishwa kwa kusisitiza uchamungu.

Hii inaonesha kuwa moja ya malengo makuu ya ibada ya Hijja ni kumuinua mja katika daraja ya uchamungu na kumjenga katika utiifu wa Mwenyezi Mungu kwa dhati.

## Kuboresha tabia njema

Watu wengi huzingatia ibada za kimwili kama sala na swaum, lakini wakati mwingine husahau umuhimu wa tabia njema. Si ajabu kumkuta mtu akifanya juhudi kubwa katika ibada, lakini ana kasoro nyingi katika maadili na uhusiano wake na watu wengine.

Hivyo, ibada ya Hijja inapaswa kuwa shule ya malezi ya tabia njema, marekebisho ya mwenendo wa maisha, pamoja na kuhifadhi na kuimarisha utambulisho wa Kiislamu.

Katika ibada ya Hijja hakuna ubaguzi wa rangi, taifa, lugha wala kabila. Waislamu wote huvaa ihramu na kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu kwa uRehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yakea.

Mwenyezi Mungu anasema: "Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke, na tumekufanyeni kuwa mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye mchamungu zaidi." [Qur'an, 49:13].

## Kuepuka mabishano yasiyo na faida

Mwenyezi Mungu anasema: "Wala hakuna mabishano katika Hijja." [Qur'an, 2:197]. Hata hivyo, baadhi ya watu wameyafanya mabishano kuwa njia yao ya kuelimishia wengine.

Badala ya kufundisha kwa hekima na kutoa mwongozo sahihi, hujihusisha na mijadala inayochochea ushindani wa hoja na kung'ang'ania misimamo binafsi.

Mazingira ya Hijja humfanya hujaji atende mambo kwa msingi wa elimu, maarifa na hekima. Aidha, humfundisha kuepuka mabishano yasiyo na manufaa – iwe katika masuala ya dini au mambo mengine ya maisha.

## Kuimarisha Tauhidi

Jambo muhimu zaidi kwa waliohiji ni kuimarisha tauhidi, yaani kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada. Hili lilionekana wazi katika talbiya, takbiri na dua mbalimbali za Hijja.

Vitendo vyote hivyo vinathibitisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kujiepusha na shirk katika aina zake zote.

## Kutukuza alama za Mwenyezi Mungu

Mwenyezi Mungu anasema: "Na anayezitukuza alama za Allah, basi hilo ni katika uchamungu wa nyoyo." [Qur'an, 22:32]. Aya hii inaonesha umuhimu wa kuheshimu na kutukuza alama na ibada zilizowekwa na Mwenyezi Mungu, jambo ambalo ni dalili ya uchamungu wa kweli.

Hivyo, baada ya kutekeleza ibada ya Hijja, mahujaji wanapaswa kushikamana na tauhidi na kujiepusha na shirk. Hawapaswi kumuomba yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, wala kuchinja, kuweka nadhiri, au kufanya ibada yoyote isipokuwa kwa ajili yake.

Vilevile, wanapaswa kuepuka kwenda kwa wachawi na makuhani au kuwaamini. Aidha, hawapaswi kutafuta baraka kwa njia ambazo hazijathibiti katika mafundisho ya Kiislamu.

## Kutubia na kuanza ukurasa mpya

Mahujaji wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia kutekeleza ibada ya Hijja. Shukrani ya kweli ni ile inayoonekana kwa ulimi, moyo na vitendo.

Miongoni mwa shukrani hizo ni kuendelea kufanya mema, kuacha maovu na kuwalingania wengine katika kheri walizojifunza wakati wa Hijja, kama vile tauhidi, Ikhlas, uchamungu na tabia njema.

Kudumu katika mema mpaka mwisho wa uhai

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Usimkosoe mwanao katika nyakati hizi



Wazazi wengi wana nia njema wanapowakosoa au kuwarekebisha watoto wao. Wanataka kuwafundisha maadili mema, kuwajenga katika nidhamu na kuwaepusha na makosa. Hata hivyo, jambo ambalo wazazi wengi hulipuuzia ni kwamba si kila wakati unafaa kwa mafunzo au ukosoaji.

Katika malezi, si maneno pekee yanayobeba uzito, bali pia muda yanaposemwa.

Wataalamu wa saikolojia ya watoto wamekuwa wakisisitiza kuwa ujumbe mzuri unaweza kupoteza thamani yake ikiwa utatolewa katika wakati usio sahihi. Mtoto anaweza kusikia maneno yako, lakini asiyaelewe au asiyapokee kwa sababu hali yake ya kihisia haimruhusu kufanya hivyo.

Hizi ni nyakati tano ambazo mzazi anatakiwa kuwa mwangalifu kabla ya kuanza kumkosoa au kumrekebisha mtoto wake.

## *Kwanza,* usimrekebishe mtoto wakati analia au amezidiwa na hisia

Mtoto anapolia, kuumia, kukasirika au kuogopa, ubongo wake huwa umejikita zaidi katika kushughulikia hisia kuliko kupokea maelekezo. Katika hali hiyo, maneno ya ushauri au ukosoaji hayana nafasi kubwa ya kufika alikokusudiwa.

Kwa mfano, mtoto akianguka na kuumia, si wakati wa kumwambia, "Nilikwambia usikimbie." Anachohitaji kwanza ni utulivu, faraja na kuhisi yuko salama. Baada ya kutulia ndipo unaweza kumfundisha somo la tahadhari au uwajibikaji. Wakati mwingine mzazi anapotanguliza ukosoaji kabla ya utulivu, mtoto hujifunza kuhusisha makosa yake na aibu badala ya kujifunza suluhisho.

## *Pili,* usimrekebishe mbele za watu

Hakuna anayependa kudhalilishwa hadharani, na watoto nao si tofauti. Kumsahihisha mtoto mbele ya wageni, marafiki zake, ndugu au wanafunzi wenzake kunaweza kuumiza heshima yake na kuathiri hali yake ya kujiamini.

Lengo la marekebisho ni kufundisha, si kuaibisha. Mtoto anapaswa kuona mzazi wake kama mtu anayemlinda, si mtu anayemsababisha aonekane mdogo mbele za wengine. Pale ambapo marekebisho yanahitajika haraka, ni busara kumwondoa pembeni na kuzungumza naye kwa utulivu kuliko kumkaripia hadharani.

Watoto wanaolelewa kwa kuheshimu utu wao mara nyingi hujenga uhusiano wa karibu na wazazi wao na huwa tayari zaidi kupokea ushauri.

## *Tatu,* usimrekebishe mara tu baada ya kushindwa.

Mtoto aliyefeli mtihani, aliyepoteza mashindano au aliyeshindwa kutimiza jambo fulani tayari anakuwa amebeba mzigo wa kihisia. Anaweza kuwa amevunjika moyo, amejilaumu au amepoteza kujiamini.

Katika wakati huo, ukosoaji mkali unaweza kuongeza maumivu badala ya kujenga suluhisho. Mtoto anaweza kuanza kuamini kwamba thamani yake inategemea mafanikio pekee. Wengine huacha hata kujaribu tena kwa kuogopa kushindwa mara nyingine.

Kabla ya kutoa maelekezo au uchambuzi wa makosa yaliyotokea, mnyanyue kwanza kihisia. Mhakikishie kuwa kushindwa ni sehemu ya kujifunza. Baada ya hali kutulia, ndipo mjadili kwa pamoja kile kilichokwenda vibaya na namna ya kufanya vizuri zaidi wakati ujao.

## *Nne,* usimkosoe mtoto kabla ya kulala.

Dakika za mwisho kabla ya usingizi zina umuhimu mkubwa katika afya ya kihisia ya mtoto. Mara nyingi ndizo kumbukumbu na mawazo yanayobaki akilini wakati wa kulala.

Mtoto anayelala akiwa ameumizwa, amekasirishwa au amedhalilishwa anaweza kuamka kesho akiwa bado amebeba hisia hizo. Hii haimaanishi makosa yapuuzwe, bali inamaanisha kuwa siku inapaswa kumalizika kwa maelewano kuliko mgogoro.

Ikiwezekana, maliza siku kwa mazungumzo ya upendo, msamaha na uhakikisho kwamba makosa yaliyotokea hayabadilishi upendo wako kwake.

## *Tano,* usimkosoe wakati anajivunia alichokifanya.

Watoto hujenga kujiamini hatua kwa hatua. Wanapokuonyesha mchoro waliouchora, kazi ya shule waliyoifanya au jambo jipya walilojifunza, mara nyingi wanatafuta kuthaminiwa kabla ya kusahihishwa.




MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Mambo 6 tunayafanya bila kujua tunachochea watu watutendee vibaya

**Watu wengi huamini kuwa wanatendewa vibaya kwa sababu ya ubaya au ukatili wa watu wanaowazunguka. Wakati mwingine hilo ni kweli. Hata hivyo, katika baadhi ya mazingira, tatizo si tu kile ambacho wengine wanafanya, bali pia ujumbe tunaoutuma bila kujua kupitia matendo yetu.**

**Hii haimaanishi kwamba mtu anayefanyiwa ubaya ndiye mwenye kosa. La hasha. Kila mtu anawajibika kwa matendo yake. Lakini ukweli ni kwamba watu hujifunza namna ya kututendea kutokana na kile tunachokubali, tunachovumilia na tunachoruhusu kiendelee bila mipaka.**

**Hizi ni ishara sita ambazo unaweza kuwa unazionesha bila kutambua, na zikawafanya wengine waamini kuwa wanaweza kuendelea kukutendea vibaya bila matokeo.**

### *Mosi:* Unanyamaza au kucheka mtu anapovuka mipaka yako

Mtu anapokudhalilisha, kukutukana au kukufanyia jambo lisilokubalika, unaweza kuamua kunyamaza ili kuepusha mgogoro. Wengine hata hucheka ili kuonesha kuwa hawajaumizwa.

Tatizo ni kwamba watu wengi hutafsiri ukimya kama kukubaliana. Wanapoona hakuna upinzani, wanaamini walichofanya hakikuwa na tatizo. Na unapocheka, hata kama ni kwa kujitetea au kuficha maumivu, unaweza kumpa mtesi ishara kuwa tabia yake imekubalika.

Mipaka isiyotetewa huonekana kama mipaka ambayo haipo.

### *Pili:* Unasamehe haraka sana kwa jina la amani

Kusamehe ni jambo jema. Lakini wakati mwingine watu hutumia msamaha kama njia ya kukwepa mazungumzo magumu.

Baada ya kutendewa vibaya, unajikuta unasema, "Ni Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yakea tu", "Sitajishusha hadi kiwango chao" au "Acha nipuuze." Unafanya hivyo ili kulinda amani na kuzuia mgogoro.

Lakini ikiwa hakuna uwajibikaji, hakuna funzo linalopatikana. Mtu anayekukosea anaweza kuona kuwa hakuna gharama yoyote ya tabia yake. Matokeo yake ni kurudia kosa lilelile mara kwa mara.

Amani ya kweli haijengwi kwa kuficha maumivu, bali kwa kuyashughulikia kwa njia sahihi.

### *Tatu:* Unaomba msamaha kwa makosa ambayo si yako

Kuna watu ambao wamezoea kubeba lawama hata pale ambapo hawana kosa lolote. Wanajikuta wakisema "samahani" ili tu hali itulie.

Unaomba msamaha kwa sababu mtu mwingine amekasirika. Unaomba msamaha kwa sababu hutaki kuonekana mgumu. Unaomba msamaha kwa sababu unathamini uhusiano kuliko haki yako.

Kadiri unavyoendelea kubeba makosa ya wengine, ndivyo unavyowafundisha kuwa wewe ndiye utakayebeba mzigo wa matokeo ya tabia zao. Mwishowe, wanazoea kutowajibika kwa sababu wanajua utajilaumu badala yao.

### *Nne:* Unapatikana muda wote bila kujali unavyotendewa

Urafiki, undugu na mahusiano yanahitaji kujitolea. Lakini kuna tofauti kati ya kujitolea na kujisahau.

Unapiga simu lakini hupigiwi. Unawatembelea lakini kila mara wana shughuli. Unatafuta muda wao lakini hawatafuti wako. Hata hivyo, wanapokuhitaji wewe, unakimbia mara moja.

Tabia hii inaweza kutuma ujumbe kuwa muda wako hauna thamani Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yakea na wao. Watu wengi hujifunza kuthamini kile wanachohofia kukipoteza. Ikiwa unapatikana kila wakati bila masharti yoyote, baadhi yao wataanza kukuchukulia kawaida.

### *Tano:* Wewe ni muelewa kupita kiasi

Huruma ni sifa nzuri. Lakini huruma isiyo na mipaka inaweza kuwa mlango wa kutumiwa vibaya.

Kila mara unatafuta sababu za kuhalalisha tabia za watu. Ukipuuzwa unasema wamechoka. Ukiahidiwa na kuachwa unasema labda walikuwa na matatizo. Ukitendewa vibaya unatafuta maelezo badala ya kutambua ukweli.

Tatizo si kuwa muelewa. Tatizo ni kutumia uelewa kama sababu ya kuvumilia mambo ambayo hupaswi kuvumilia.

Wakati mwingine maelezo yanaweza kueleza tabia, lakini hayaipaswi kuhalalisha tabia hiyo.

### *Sita:* Unaweka furaha ya wengine mbele ya yako kila wakati

Baadhi ya watu wamefundishwa kuwa kujifikiria ni ubinafsi. Hivyo hujitahidi kuhakikisha kila mtu mwingine ana furaha hata kama wao wenyewe wanateseka.

Unaahirisha mahitaji yako ili kuwafurahisha wengine. Unaogopa kusema hapana kwa sababu hutaki mtu akasirike. Unabeba mizigo ambayo si yako kwa sababu unaogopa kuonekana mbaya. Lakini ukweli ni kwamba watu wengi hawataheshimu mahitaji yako ikiwa wewe mwenyewe huyaheshimu.

Mara nyingi watu hawatendi vibaya kwa sababu ni makatili. Wanafanya hivyo kwa sababu hawajawahi kuoneshwa mpaka unaoonesha mwisho wa kile unachoruhusu. Mipaka si ukatili. Mipaka ni kujiheshimu.

Mwisho wa siku, watu watakutendea kulingana na kile wanachoamini utakikubali. Ndiyo maana kujifunza kusema hapana, kutetea heshima yako na kuweka mipaka si ubaya. Ni sehemu muhimu ya kujilinda na kujenga mahusiano yenye afya. Wema ni sifa nzuri, lakini